epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Aprili 25, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581657
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22
GIROUD ATIMKIA MAREKANI

**LHRC** yashauri itungwe sheria kulinda watoto na wanawake UKURASA 3

**Mtaalamu** ataja mbinu za kukabili mafuriko UKURASA 4



**Wachimbaji** wadaiwa kutembeza kichapo, kuchoma moto ofisi UKURASA 4

# Hoja 16 THTU uboreshaji wa kikokotoo, NHIF

UKURASA 2



Dk. Paul Loisulie



Rais Samia Suluhu Hassan akionyesha kitabu cha Safari za picha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka 60, baada ya kukizindua kabla ya kumkabidhi Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Rais Samia asema historia chachu maendeleo ya utalii na uchumi

UKURASA 3

## Misaada mafuriko Rufiji yazua jambo, DC atoa neno

UKURASA 2






MIAKA 60 YA MUUNGANO

OFA KATIKA TOLEO MAALUM!!

Katika kuadhimisha Siku ya Muungano mwaka huu, tarehe 26 April 2024 Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya Nipashe na The Guardian Itatoa toleo maalum la Muungano, hivyo inawakaribisha kutoa salamu za kumbukizi, matangazo, picha na makala za mafanikio katika kusherekea miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa PUNGUZO MAALUM

Wahi mapema kwa sikukuu hii upate PUNGUZO, Artwork ya bure na nafasi katika majukwaa yetu ya kidigitali.

*vigezo na masharti kuzingatiwa*

The Guardian Nipashe

KWA MAWASILIANO TUPIGIE | +255 677 020 701

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz Au Tutembelee The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Mkabala na ITV / Radio One, Dar es Salaam
Tovuti: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com



Wanafunzi wa kike waliofanya vizuri masomo ya sayansi katika mitihani ya kidato cha pili mwaka 2023 kutoka shule za sekondari za mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wakipata mafunzo kutoka kwa Meneja Matengenezo wa kampuni ya Vodacom Tanzania PLC, mkoa wa Mbeya, Adam Mndeme (kushoto), walipotembelea kituo cha kupokelea mawasiliano cha kampuni hiyo, jijini Mbeya juzi, ziara iliyoandaliwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (USCAF), ili kuwajengea wasichana uelewa kuhusu masomo ya Sayansi, Uhandisi, Tehama na Hisabati. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hoja 16 THTU uboreshaji wa kikikotoo, bima ya afya

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

IKIWA zimesalia siku kadhaa kufikia maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi (Mei Mosi), Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu (THTU), kimefanya uchambuzi na kutoa mapendekezo 16 kuhusu hoja za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na kikokotoo cha mafao ambacho kimekuwa kikilalamikiwa na watumishi wa umma nchini.

Mwenyekiti wa THTU Taifa, Dk. Paul Loisulie, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, alisema vikwazo vilivyopo kwenye mfuko huo na pensheni vinaathiri haki za mfanyakazi kupata stahiki husika pindi anapostaafu.

Kuhusu kikokotoo, Dk. Loisulie alisema kanuni inayotumika haiakisi hali halisi ya wanachama kwa kanuni 8(1) (a) (b) (c) inayozungumzia kigezo cha umri na malipo ya mkupuo. Alisema wakati umri wa kuishi wa Mtanzania umeongezeka, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na makazi ya Mwaka 2022, mafao kwa mkupuo kwa mwanachama yanakuwa ni madogo.

"Madhara yake ni kwamba kupunguza umri wa kuishi baada ya kustaafu kunapunguza pensheni ya mwanachama na kupungua kwa morali ya wanachama na watu kukimbia utumishi wa umma," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alipendekeza kikokotoo kifanyiwe mabadiliko kwa kuongeza umri baada ya kustaafu kutoka miaka 12.5 hadi 15.5 na wanachama wapewe angalau asilimia 50 kama mafao ya mkupuo. Pia alishauri itumike kanuni ya 1/540 badala ya 1/580.

Pia alisema THTU imebaini waziri husika ana mamlaka ya kuamua kiwango cha michango ya mwanachama katika mfuko kupitia kifungu Na. 18, hivyo mamlaka aliyopewa waziri yakitumiwa vibaya yatakuwa kandamizi kwa wanachama.

Alipendekeza kifungu kidogo cha 18(2)(b) kiondolewe na kionyeshe kuwa waziri hapaswi kuwa na mamlaka ya kupanga michango ya wanachama.

Kadhalika, alisema kifungu na 39 kinachohusu wajane, wagane na watoto wana haki ya kunufaika na mafao ya mwanachama aliyekuwa wakimtegemea kwa muda wa miaka mitatu pekee kutoka tarehe ya kifo cha mwanachama, kinasababisha familia kukosa huduma stahiki na kupendekeza walipewe angalau kwa miaka 15.

"Kifungu cha 18 (a) kinamyima mnufaika haki yake ya kikatiba ya kuoa au kuolewa, Neno until "re-marriage" linapaswa liondolewe ili kulinda haki ya kikatiba ya kuoa au kuolewa pasipo na vikwazo. Mjane,mgane aruhusiwe kupata mafao bila ya vikwazo vya umri na kuwa na mtoto," alisema.

Pia alisema kifungu na 40 kuhusu wanachama katika mfuko mmoja kuwa na kanuni tofauti za kukokotoa mafao ni kutengeneza matabaka katika jamii na kupendekeza kuwepo na masharti yanayofanana kwa wanachama wote ili kuondoa ubaguzi na kigezo cha mshahara mkubwa kitumike kwenye mafao.

Kuhusu mwanachama kupunjwa mafao kwa kosa la mwajiri, alisema kifungu cha 20 kinazungumzia Mwajiri anaposhindwa kuwasilisha michango ya mwanachama kwa wakati au kutowakilisha kabisa. Kifungu hakimlindi mwanachama iwapo mwajiri amechelewesha au hakupeleka michango kwenye mfuko na kusababisha kupunjwa mafao.

"Tunapendekeza kiongezwe kifungu kidogo maalum kitakacholinda haki za mwanachama moja kwa moja iwapo mwajiri atachelewesha au kutopeleka mchango wa mwanachama katika mfuko na mwanachama alipwe mafao yake yote na mfuko umdai mwajiri michango iliyokosekana pamoja na penati,"alisema.

**MAPENDEKEZO NHIF**

Alisema kifungu 16(3) cha Sheria ya Bima ya Afya kinamtaka mnufaika kuchangia gharama za ziada za matibabu lengo likiwa ni kuuondolea mfuko wajibu wake wa kisheria wa kulipia gharama za matibabu. Alisema hali hiyo inampa mwanachama mzigo na inaathiri huduma ya matibabu kwa mnufaika, hivyo kumfanya kutokuona umuhimu wa kuwa na bima ya afya.

"Kifungu cha 16(3) cha Sheria ya Bima ya Afya kiboreshwe kwa kuupa mfuko wajibu wa kumlipia mwanachama huduma zote stahiki kutokana na mahitaji ya ugonjwa wake kwa ubora unaostahiki," alisema.

Kuhusu mabadiliko ya wigo wa upatikanaji wa huduma ya bima mara kwa mara, alipendekeza Kifungu cha 16(4) cha Sheria ya Bima ya Afya kirekebishwe kwa kutaka mabadiliko ya vitita vya matibabu yafanyike kwa kuwashirikisha wadau ambao ni watoa huduma na wanufaika au wachangiaji.

Alipendekeza miongozo ya upangaji wa gharama za matibabu iwe shirikishi na izingatie uhalisia wa utoaji wa huduma husika na mchangiaji apewe uhuru wa kuamua wategemezi anaotaka wanufaike na bima bila kuathiri ukomo wa idadi kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 3 cha sheria ya Bima ya Afya.

Alisema kunahitajika majadiliano kutokana na kutokuwa na usawa katika kupata huduma kwa wanufaika wa huduma ya bima, yaani wabunge na watumishi wa umma.

"Tunapendekeza mfuko ufuate matakwa ya kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Bima ya Afya ambacho kimetaja makundi ya watu wanaoweza kujiunga na Bima ya Afya ambaio ni watumishi wa umma, wenza wao, Watoto au wategemezi, wastaafu na madiwani.

"Hata hivyo, kinyume cha sheria inavyotaka, kwa sasa sheria imeongeza wigo wa wanachama wa Bima ya afya kama vile wabunge, mashirika binafsi, watoto, wanafunzi wa vyuo,"alisema.

Alipendekeza Mfuko uwashirikishe wadau kikamilifu wakati wa upangaji wa gharama za huduma na kuwe na chombo mahsusi cha kudhibiti gharama za huduma za bima za afya.

"Tunashauri tathmini ifanyike ili kuona kama viwango vya michango inayotolewa sasa ina uhalisia na gharama za matibabu wanazopata wanufaika. Tunashauri serikali iweke tengo maalum kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato kutoka kwenye rasilimali tulizonazo ili kuutunisha na kuuimarisha Mfuko," alisema.

# Misaada waathirika mafuriko Rufiji yazua jambo, DC ajibu

**Na Elizabeth Zaya**

BAADHI ya waathirika wa mafuriko katika vijiji vilivyoko kata ya Muhoro, Rufiji mkoani Pwani, wamelalamikia utaratibu wa utoaji wa misaada ya chakula iliyopelekwa na serikali na wadau mbalimbali.

Kutokana na malalamiko hayo, Mkuu wa Wilaya ya Rufuji, Meja Edward Gowele, amefafanua madai hayo huku akiahidi kuchukua hatua kali dhidi ya wahusika.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya waathirika hao walisema utaratibu wa ugawaji wa misaada hiyo ya chakula hususani katika ngazi za vijiji waliko waathirika hao haiwafikii baadhi ya walengwa huku wengine wakidai kuwa unafanywa kwa kujuana katika ngazi za vijiji.

Pia walisema hata wachache wanaofikiwa, kiwango wanachopewa hakitoshelezi kulingana na ukubwa wa familia au kaya kwa sababu hata kinapogawiwa kidogo muda wa kuzirudia kaya hizo haujawekwa vizuri.

Walisema hatua hiyo inachangia baadhi ya familia kuishi katika wakati mgumu na kutokuwa na uhakika wa chakula kila siku.

Jambo lingine lililobainishwa na waathirika hao ni kwamba kwa wale ambao wako katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wamekuwa wakiambiwa hawahusiki na misaada hiyo ya chakula licha ya kwamba wameathirika na mafuriko hayo.

Mohamed Seleman, mkazi wa kijiji cha Chela katika Kata ya Muhoro, alisema utaratibu wa ugawaji chakula hicho ni wa kibaguzi.

"Utaratibu wa ugawaji ni mbovu sana. Kwanza wananchi hatushirikishwi kwamba siku gani chakula kitagawiwa. Huwa wanashtukiza tu na ukienda unaambiwa wanagawa kwa watu wachache. Siku moja nimeenda nikaambiwa leo ni watu 10 tu kwa hiyo nikawa nimekosa.

"Wameshagawa awamu nne lakini binafsi na familia yangu hatujabahatika hata siku moja, yaani nimepanga foleni, anapata mwenzangu mimi nakosa. Yaani wanatumia ujanja fulani hivi wa kujuana wakati wanagawa," alisema.

Said Mbonde, mkazi wa kijiji cha Mohoro, alisema yeye ana familia ya watu sita lakini tangu akutwe na maafa hayo, amepatiwa kiroba kidogo cha unga na mpaka sasa hajapata tena na kila akienda wanamfukuza.

"Mpaka jana (juzi), nimekwenda walipokuja lakini nikafukuzwa, wanasema tayari mimi nilishapewa. Sasa hicho kiroba walichonipa kwa mara ya kwanza ndicho bado kipo mpaka sasa?" alihoji Mbonde.

Hamidu Kassim, mkazi wa kijiji cha Kipoka katika kata ya Mohoro, alisema utaratibu wa ugawaji vyakula hivyo si wa haki.

"Tunaona misaada mingi inaletwa kwa ajili ya maafa lakini tumeshuhudia utaratibu wa ugawaji kutufikia waathirika si mzuri. Hatujui wanazingtia ukaribu, kujuana pasipo kuangalia waathirika wote kwamba wanahitaji msaada au nini.

Lakini la kusikitisha zaidi tuna wenzetu walio kwenye mpango wa TASAF ambao nao wameathirika na wenyewe wanapokwenda kupanga foleni pale wanapotoa misaada wanafukuzwa. Wanaambiwa wao haiwahusu kwa sababu wanapatiwa na mfuko huo," alisema Kassim.

Fatma Sultan, alisema yeye baada ya nyumba yake kuzama na mafuriko anahifadhiwa kwenye nyumba ya jirani, hivyo anapokwenda kufuata msaada huo wa chakula amekuwa akiambiwa hastahili kwa sababu tayari amepata hifadhi.

"Nimesumbuliwa sana kila siku nikienda nafukuzwa, lakini nimekuwa sichoki kuwasumbua, kila wanapokuja huwa nakwenda kuwaambia wananiweka kwenye fungu gani kwa sababu nina hali ngumu kama waathirika wengine kwa hiyo jana (juzi), ndio nikabahatika kupewa kilo tatu za mchele na unga pamoja na maharagwe nusu wakaniambia nisirudi tena," alisema Fatma.

Akizungumza baada ya kuwatembelea baadhi ya waathirika katika kijiji cha Muhoro, Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, alisema serikali inapaswa kuwagawia chakula wananchi wote walioathirika na mafuriko katika eneo hilo kwa usawa.Akijibu malalamiko hayo baada ya kuulizwa na Nipashe, Meja Gowele alisema endapo watabaini kuna mtendaji anagawa chakula kwa ubaguzi, atachukuliwa hatua.

"Wa kwanza wanaogawiwa ni wale walioko kwenye makambi, wa pili ni wale ambao wamepokea kaya kwenye familia zao na tatu ni watu wenye hali duni ya maisha. Ingawa wote tumeathirika, tutachambua namna hiyo kwa kufanya tathmini ya kina," alisema.

HABARI KITAIFA

# Samia asema historia chachu kukuza utalii

Na Paul Mabeja, DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema kuna haja ya kutumia historia mbalimbali zilizopo nchini ili kukuza utalii na kuongeza pato la taifa kama ambavyo mataifa mengine yanafanya duniani.

Rais Samia alisema hayo jana Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma kwenye hafla ya utoaji wa nishani za Muungano pamoja na uzinduzi wa vitabu vya Historia ya Muungano na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Alisema kama historia zilizopo nchini zitawekwa vizuri, zitasaidia kukuza utalii kama ambavyo mataifa mengine yamekuwa yakifanya na kuyaingizia mapato na hatimaye kukuza uchumi.

"Wenzetu wanatumia historia za mataifa yao kukuza utalii. Watu wanatoka katika mataifa mengine kwenda kujifunza historia ya taifa lingine, hivyo basi kama historia ya taifa letu, ikiwamo hii miaka 60 ya Muungano tutaitumia vizuri, tutakuza utalii.

"Nilikuwa Uturuki hivi karibuni, wenzetu wanatumia historia ya taifa lao watu kwenda kutalii kujifunza namna ambavyo walipigana vita wakapata eneo lakini pia baadaye wakapokonywa," alisema.

Pia aliwataka Watanzania kuendelea kudumisha amani, mshikamano na uzalendo kulinda Muungano ambao mwaka huu unatimiza miaka 60.

"Pia nitoe wito kwa Watanzania kusoma vitabu hivi ili kuenzi kazi nzuri iliyofanywa. Lakini kusoma vitatu hivi itasaidia watu kujua historia na magumu ambayo Muungano wetu umepitia kwa sababu hata katika baraza la mawaziri, kuna vitu nikiuliza vya kimuungano, watu wanakosa majibu. Vitabu hivi vitasaidia kutupa uelewa kwani wengi wamezaliwa baada ya Muungano," alisema.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliipongeza timu iliyofanikisha uandishi wa vitabu hivyo ambavyo vitasaidia kuongeza uelewa kwa Watanzania na wageni.

"Zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wamezaliwa baada ya Muungano, hivyo vitabu hivi ni nyenzo muhimu kusaidia watu kuufahamu muungano wetu," alisema. Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema vitabu hivyo vinabeba historia kubwa ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa taifa la Tanzania yakiwamo mafanikio na changamoto zake.

Alisema vitabu hivyo vikatumike kuwajengea uelewa watoto na watu wote ambao wamezaliwa baada ya Muungano ili waufahamu na kuulinda kikamilifu. "Lakini pia tunao wajibu sisi kama taifa kuendelea kuwakumbuka na kuwaenzi viongozi wetu wote waasisi wa Muungano huu," alisema

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo alisema kupitia vitabu hivyo, Watanzania watapata fursa kuuelewa Muungano kwa kuwa bado watu wengi hawana uelewa wa kutosha.

"Vitabu hivi vimeeleza mambo mengi sana ikiwamo wasifu na mambo ambayo yalifanywa na viongozi waliowahi kuhudumu kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais tangu mwaka 1964," alisema.

Alisema tangu Muungano uanze mwaka 1964 hadi leo, Makamu wa Rais 14 wamehudumu katika ofisi, tisa wakitoka Zanzibar na watano Tanzania Bara na kati ya hao, mwanamke ni mmoja tu kwa miaka yote 60 ya Muungano.

# LHRC yashauri sheria itungwe kuwalinda wanawake na watoto

Na Enock Charles

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimependekeza kutungwa sheria kulinda makundi maalum wakiwamo wanawake na watoto dhidi ya ukatili.

Mapendekezo hayo yanatokana na taarifa ya kituo hicho kwa mwaka 2023 kuonyesha kuwa makundi hayo ndiyo yaliyoathirika zaidi dhidi ya vitendo hivyo.

Akizungumza katika uzinduzi wa Ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2023, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, alibainisha kuwa robo tatu ya manusura wa ukiukwaji wa haki za binadamu walikuwa watoto asilimia 45 na wanawake asilimia 30, huku manusura wengine wakiwa ni wazee (asilimia 12) na watu wenye ulemavu.

"Watoto na wanawake ni waathirika wakubwa wa ukiukwaji wa haki za binadamu na baadhi ya mikoa ambayo imeongoza kwa ukiukwaji wa haki hizo ni Dar es Salaam, Njombe, Geita, Arusha, Kilimanjaro, Mara, Kigoma na Dodoma" alisema Dk. Henga.

Kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo, Dk. Henga alitaka jamii kutokufumbia macho pale inapoona ukatili na ukiukwaji wa haki za binadamu vinafanyika hasa kwa Watoto.

Alisema mara nyingi vitendo hivyo hufanywa na watu wa karibu na mtoto kama vile mjomba, baba, baba mdogo, babu hata mama mzazi, hivyo kuwa vigumu kuripotiwa katika vyombo vya ulinzi na usalama.

Ripoti hiyo pia ilifichua kuongezeka suala la mauaji ya kujichukulia sheria mkononi kwa wananchi wanaokamatwa kwa makosa mbalimbali yakiwamo ya wizi pia mauaji ya wenza kwa kile kinachodaiwa wivu wa kimapenzi na imani za kishirikina.

"Masuala mengine yaliyoainishwa katika ripoti hii ni mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina na mauaji ya wenza baina ya wenza hao kwa mmoja kumuua mwenzie kwa wivu wa mapenzi," alisema Dk. Henga

Mbali na haki za watoto na wanawake, ripoti hiyo ilibainisha pia ukiukwaji wa haki katika kundi la waandishi wa habari ukiwamo wa kiuchumi kwa kutokupewa mikataba ya kazi na fedha zao kutokupelekwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii huku wengine wakilipwa ujira mdogo wa kazi zao, hivyo kutaka waajiri kujirekebisha.

Nipashe MWANGA WA JAMII
The Guardian www.ippmedia.com

Kutoka Menejimenti ya The Guardian Limited



Wapendwa Wateja wetu

Tunayo furaha kutangaza hatua kubwa kuelekea upatikanaji wa magazeti yetu kidijitali. Kuanzia tarehe 13 Aprili 2024, magazeti ya wikiendi ya **Nipashe Jumamosi, Nipashe Jumapili na The Guardian on Saturday** yanapatikana kwa njia ya gazeti-mtandao kupitia **epaper.ippmedia.com** au **www.ippmedia.com**

Siku za wiki (Jumatatu hadi Ijumaa) utaendelea kufurahia matoleo yote, kuchapishwa na Mtandaoni

Asante kwa usomaji wako, na kuendelea kuwa nasi katika mabadiliko haya.

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701
Subscription: 0625 174 714
Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

# Mtaalam aanika mbinu kukabili mafuriko

**Na Jenifer Gilla**

MTAALAM wa mabadiliko tabianchi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Pius Yanda, ameishauri serikali kupanua mitaro ya barabarani iwe na uwezo wa kusafirisha maji yanayotiririka kwa kiasi kikubwa ili kuepuka mafuriko yanayojitokeza na kuathiri wananchi.

Pia ametoa ushauri huo wakati maeneo mengi nchini hasa mikoa ya Kanda ya Pwani, yaani Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Lindi na Mtwara kukumbwa na mvua kubwa iliyosababisha maafa kwa binadamu na uharibifu wa miundombinu huku zaidi ya watu 60 wakifariki dunia.

Alisema wakati mitaro hiyo inajengwa kasi ya mvua haikuwa kubwa, hivyo kuna haja ya kuipanua ili kuhimili kubeba maji yanayoendana na kiwango cha mvua kinachonyesha sasa.

"Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, mvua si nyingi zinanyesha kwa muda mfupi, lakini zinanyesha kwa kiwango kikubwa na kusababisha mitaro kuzidiwa hivyo kunatokea mafuriko kama tunayoyashuhudia sasa," alisema.

Prof. Yanda aliishauri pia serikali kupitia idara za mipango miji katika halmashauri kuanza kufikiria kujenga majengo yanayofaa kulingana na jiografia ya eneo husika, ili kuwapo na nafasi ya kutosha kupisha mkondo wa asili wa maji kupita na kuepuka mafuriko.

Alisema tatizo la mafuriko pia linachangiwa na wananchi kujenga katika maeneo ambayo ni mkondo wa asili wa maji hivyo mvua zinaponyesha yanakosa njia ya kupita na kuishia kujaa barabarani na kwenye makazi ya watu.

Pia alitaja maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo hupelekea watu kujenga nyumba za kisasa zilizosakafiwa na kuwekwa 'tiles' hivyo maji hukusanywa juu ya sakafu badala ya kunyonywa ardhini kama ilivyokuwa hapo awali.

Mtaalamu huyo wa mazingira pia alitaja usimamizi usiojitosheleza wa taka ngumu kusababisha kuzagaa mitaani na kuishia kwenye mitaro ambayo huziba na kushindwa kupeleka maji maeneo yanayofaa na kushauri manispaa kulisimamia ipasavyo suala hilo.

Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Dar es Salaam, Geofrey Mkinga, alisema ili kumaliza tatizo hilo kunahitaji juhudi za pamoja za taasisi husika kama vile Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Manispaa zote.

Alisema kwa upande wao, wanapunguza madhara kwa kusafisha na kuzibua mitaro iliyopo barabarani ingawa mitaro hiyo inazidiwa kwa kuwa maji yanakosa njia ya kupita baada ya mkondo wake kuzibwa na makazi ya watu.

Alishauri pia manispaa kusimamia zoezi la ugawaji wa viwanja ili kuhakikisha wananchi hawajengi maeneo ambayo ni mikondo ya asili ya maji kwa kuwa ni moja ya sababu za mafuriko.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Manispaa ya Kinondoni, Aquilinus Shinduki, alisema kama manispaa jukumu lao kubwa ni kuhakikisha kuwa wanasimamia taka zisimwagwe kwenye mitaro hivyo wanaendelea kutoa elimu kwa jamii.

"Kwa mfano sisi Manispaa ya Kinondoni tumetenga fungu kwa ajili ya kuzibua mitaro katika eneo letu, na ni suala ambalo ni endelevu kwa hiyo tunaamini kadiri siku zinavyoendelea tutapunguza adha hii kwa kiasi kikubwa" alisema.


Alisema pia Idara ya Mipangomiji inaendelea kusimamia na kuzuia ujenzi wa holela hasa kwenye kuwahamasisha wananchi waliojenga kwenye mabonde na pembezoni mwa mito kuhama ili maji yapite kwa uhuru na kuepusha mafuriko yanayoleta maafa kwa jamii.

TAARIFA TMA

Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) imetoa angalizo la kuendelea kuwapo na mvua kubwa kwa baadhi ya mikoa nchini ikiwamo Dar es Salaam, Tanga na Pwani na visiwa vya Unguja na Pemba mpaka kesho.

Katika angalizo la kuwapo upepo mkali unaofikia kilomita 40 kwa saa na mawimbi makubwa yanayofika mita mbili kwa baadhi ya maeneo ya Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi.

Mamlaka hiyo ilieleza kuna uwezekano wa kutokea athari ikiwamo vifo, uharibifu wa miundombinu, nyumba kujaa maji na watu kukosa makazi na kuwaelekeza watu kuchukua tahadhari.




Mwenyekiti wa Baraza la Kutokomeza Malaria Tanzania (EMCT), Leodgar Tenga (kushoto), akipongezana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi kufuatia ushirikiano baina ya pande hizo mbili katika utekelezaji wa pamoja wa adhima inayolenga kutokomeza kabisa ugonjwa wa malaria ifikapo mwaka 2030, wakati wa mkutano wa baraza hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wachimbaji wadaiwa kutembeza kichapo, kuvunja ofisi ya mtendaji

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu Mwakitolyo Na. 5, wilayani Shinyanga, wamedaiwa kufanya vurugu kwa kuwapiga raia wa China, kuvunja ofisi na kuchoma moto pikipiki ya mtendaji wa kata.

Inadaiwa kuwa wachimbaji hao wamefanya hivyo wakihofia kunyang'anywa mlima ambao hutumia kuchimba madini.

Vurugu hizo zilitokea juzi majira ya saa 11:00 jioni wakati raia hao kutoka China wakiwa na mkalimani wao, walipotembelea mlima ambao hutumiwa na wachimbaji wadogo kuchimba dhahabu, hivyo kuhofia huenda kuna mipango ya kunyang'anywa ndipo wakaanza kutembeza kichapo.

Mtendaji wa Kata ya Mwakitolyo, Raymond Jerome, akizungumza na Nipashe jana, alisema raia hao kutoka China wakiwa na mkalimani wao, hawakupita kwenye ofisi za kata bali walikwenda moja kwa moja kwenye mlima huo, ndipo wachimbaji wakajikusanya na kuwavamia huko huko mlimani na kuanza kuwapiga. Alisema baada ya vurugu hizo, wakiwa viongozi wa eneo hilo, ilibidi wafike eneo la tukio ili kuwanusuru na baada ya hapo wakawafungia kwenye ofisi za wachimbaji wakati wakiendelea kutuliza vurugu.

Jerome alisema wakiwa ndani ya ofisi hizo, wachimbaji walianza kuivunja huku wakichoma moto pikipiki yake ambayo ilikuwa nje ya ofisi, wakiwataka raia hao wa kigeni lakini bahati nzuri walifanikiwa kuwatorosha na kuwakimbiza kwenye zahanati ya Mwakitolyo ili wapatiwe matibabu kutokana na majeraha waliyokuwa nayo.

"Wachina hawa walikuwa wengi lakini baada ya vurugu hizo ,wengine walikimbia na kubaki wawili na mkalimani wao ndio waliopigwa na kujeruhiwa vibaya," alisema Jerome.

Pia alisema wakati vurugu zinaendelea, polisi walifika eneo la tukio na kuanza kupiga mabomu ya machozi ili kuwatawanya wachimbaji na kwamba hali ya amani bado haijakaa sawa.

Meneja wa Wachimbaji Wadogo wa Mwakitolyo Namba Namba 5, Leonard Waziri, alisema walishaghaa kuona raia hao wa China wakitembelea kwenye mlima ambao huchimba madini ndipo wachimbaji wakaingiwa na wasiwasi huenda wanataka kuporwa mlima wao, hivyo kuanzisha vurugu na kuwapiga na kufikia hatua ya kuvunja ofisi na kuchoma moto pikipiki ya mtendaji.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kennedy Mgani, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba baadhi ya wachimbaji ambao walianzisha vurugu hizo na kuwapiga raia hao wa China, wanasakwa na wakikamatwa watachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema hali za Wachina hao zinaendelea vizuri baada ya kupatiwa matibabu na kuonekana hawakujeruhiwa sana hadi kufikia hatua ya kulazwa.

## Leseni, matumizi kikoa cha taifa vyaongezeka

**Na Mwandishi Wetu**

LESENI za huduma za utangazaji Tanzania zimeongezeka kati ya asilimia tano na 350 kwa aina tofauti kati ya Desemba 2023 na Machi 2024, huku taasisi zaidi zinatumia kikoa cha Tanzania kwenye mawasiliano yao mtandaoni, taarifa ya hivi karibuni imeonesha.

Taarifa ya hali ya sekta ya mawasiliano iliyotolewa jana Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari, inaonyesha kuwa leseni za usafirishaji vifurushi kati ya miji kwenye mikoa zimeongezeka kwa asilimia 30 ni za mabasi ya abiria. Ripoti hiyo imeeleza kuwa leseni za kitaifa za huduma za maudhui ya televisheni za kulipiwa (shitariki) ziliongezeka kwa asilimia 60 kutoka 10 hadi 16 na leseni za wilaya kwa kundi hili zimeongezeka kwa asilimia 350 kutoka mbili hadi tisa kati ya Desemba, 2023 na Machi, mwaka huu.

"TCRA ilitoa leseni 17 za redio za jamii kati ya Januari na Machi 2024, kulinganisha na 11 kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2024 ambazo ni ongezeko la asilimia 55. Leseni hii inawezesha utoaji huduma za utangzaji mwa jamii au watu waliojumuika sehemu moja kijiografia," alisema.

Kwa mujibu wa kanuni za maudhui ya redio na televisheni, watangazaji wa kundi la leseni za jamii wanatoa kwa jamii husika maudhui yanayohusu masuala ya jamii hiyo ambayo kwa uzoefu hayatolewi na watoa huduma wengine wa maudhui wanaofikisha huduma maeneo vilipo vituo vya jamii.

Aidha, taarifa hiyo ilionyesha kuwa vikoa vya taifa vinavyoishia na dot 'tz' vilivyosajiliwa vimeongezeka kutoka 29,006 mwishoni mwa Desemba 2023 hadi 29,968 mwishoni mwa Machi, 2024. "Taasisi na watu binafsi wanazidi kutumia kikoa cha Tanzania kwenye vovuti zao na barua pepe.Kikoa ni jina mahsusi linalotambua raslimali za intaneti kama vile tovuti zilizosajiliwa kwenye nchi husika na ngazi nyingine duniani,"alisema.

Pia ilibainisha kuwa vikoa vya kampuni na biashara (dot 'co'), taasisi za elimu zenye ithibati (dot 'ac') na mashirika yasiyotegemea faida kwenye shughuli zao (dot 'or') zimeongezeka zaidi kipindi hicho.

"TCRA inahimiza matumizi ya kikoa cha taifa kinachoishia na kifupisho cha Tanzania, yaani dot 'tz" kwenye maelezo na shughuli za taasisi. Vikoa vya taifa vina faida zaidi ya vile vya jumla kwa kuwa vinatambulisha taasisi na nchi husika. Vilevile vinajenga imani ya watumiaji wa tovuti ya mwenye kikoa,"ilisema taarifa hiyo.

HABARI KITAIFA

# Biteko: Uzalishaji umeme haukidhi mahitaji

**Na Vitus Audax,** DODOMA

SERIKALI imesema licha ya ongezeko la uzalishaji umeme kwa asilimia 14.2 katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, mwaka huu, bado kiwango hicho hakikidhi mahitaji ya taifa, ambayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi kutokana na ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alisema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2024/25.

Katika makadirio hayo, Dk. Biteko aliliomba bunge kuidhinisha Sh. trilioni 1.883 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za wizara hiyo.

Biteko alitaja sababu zingine za upungufu wa umeme kuwa ni pamoja na upungufu wa maji na gesi asilia katika vituo vya kufua umeme, hitilafu katika mitambo ya uzalishaji na kufanyika kwa matengenezo katika mitambo ya uzalishaji wa nishati hiyo.

Alisema mahitaji ya juu ya umeme nchini yamekuwa na kufikia megawati 1,590.1 zilizofikiwa Machi 26, mwaka huu, sawa na ongezeko la asilimia 8.1 ikilinganishwa na megawati 1,470.5 zilizofikiwa Juni 12, 2023.

**MAFANIKIO**

Dk. Biteko alisema hadi Machi, mwaka huu, hali ya uzalishaji wa umeme imependa kwa asilimia 14.2 ikiongezeka kutoka megawati 1,872.1 hadi megawati 2,138 kutokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme unaoendelea nchini kutoka umeme uliounganishwa katika gridi ya taifa.

Alisema katika kiasi hicho, megawati 836.3 sawa na asilimia 39.1 ni umeme unaotokana na nguvu ya maji, megawati 1,198.8 sawa na asilimia 56.1 unatokana na gesi asilia, megawati 92.4 (asilimia 4.3) mafuta mazito na magawati 10.5 (asilimia 0.5) ni kutokana na tungamotaka (biomass).

"Ongezeko la uwezo wa uzalishaji wa umeme limetokana na kuanza kwa uzalishaji wa umeme kupitia Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115. tayari uzalishaji umeanza kwa megawati 235 kupitia mtambo mamba tisa. Matarajio ni mradi huu kukamilika Desemba, 2024 kwa mitambo yote minane yenye uwezo wa kuzalisha megawati 235 kila moja kuwa inazalisha umeme.

"Vilevile kukamilika kwa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rusumo ambao unachangia megawati 26.7 katika gridi ya taifa, kukamilisha ujenzi wa mitambo ya kufua umeme ya Kinyerezi I Extension megawati 185. kwa sasa mitambo yote minne inafua umeme kiasi cha megawati 40 kila mmoja, hivyo kuwezesha uzalishaji wa umeme kuingizwa katika gridi ya taifa," alisema. Pia alitaja ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa jua mkoani Shinyanga wa megawati 150 unaendelea na kuwa matarajio ni umeme huo kuanza kuzalishwa ifikapo Januari, 2025.

Aidha, alisema hadi kufikia Machi 2024, uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme ambayo haijaungwa katika gridi ya taifa ni megawati 33.4 ambazo zinajumuisha mitambo inayomilikiwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCOO yenye uwezo wa kufua megawati 28.4 na megawati tano zitokanazo na nguvu ya jua kutoka kwa mzalishaji binafsi.

Biteko alisema wizara kupitia TANESCO inanunua umeme wa megawati 31 kati ya hizo 21 kutoka Uganda kwa ajili ya mkoa wa Kagera na zingine 10 kutoka Zambia kwa ajili ya mkoa wa Rukwa.

Alisema serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi mingine ya kuzalisha umeme ikiwa ni pamoja na Malagarasi (megawati 49.50, Ruhudji (megawati 358), Rumakali (megawati 222) Kakono (megawati 87.8) na Kikonge megawati 321 na utekelezaji wake umefikia katika hatua mbalimbali.




## Serikali yabanwa mikopo 'kausha damu'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SAKATA la mikopo inayolalamikiwa, maarufu kama 'kausha damu', limeendelea kuibuka bungeni huku wabunge wakihoji mikakati ya serikali wa kuzibana taasisi zinazotoa mikopo kwa riba kubwa hali inayosababisha magonjwa ya afya ya akili na uvunjifu wa ndoa.

Aidha, Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson ameiagiza Wizara ya Fedha kutafuta uhakika kama kuna kampuni za simu nchini zinatoa mikopo ya aina hiyo.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Felista Njau, alihoji mkakati wa serikali wa kukomesha mikopo ya kausha damu ili kunusuru wananchi ambao wamekuwa wakipata matatizo ya afya ya akili na ndoa nyingi kuvunjika. Katika swali la msingi, Mbunge huyo alitaka kujua kuna mkakati gani kufuatilia na kuchukua hatua kwa taasisi za fedha zinatoa mikopo yenye riba kubwa kinyume cha muongozo wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Pia Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Shally Raymond, alisema pamoja na sheria ya BoT ya mwaka 2018 na kanuni za 2019 lakini mikoa zaidi ya 17 ukiwamo wa Kilimanjaro hasa wilaya ya Moshi vijijini imekuwa ikitolewa mikopo kausha dam una kuhoji serikali inatoa kauli gani.

"Kampuni za simu zimekuwa zikitoa mikopo haraka bila kujaza fomu na vijana na wanawake wajasirimali wa Kilimanjaro wamekuwa wakichangamkia fursa hiyo lini serikali italazimisha kampuni hizo kutoa elimu," alisema.

Kutokana na kauli hiyo, Spika Tulia alisema hana uhakika kama kampuni za simu ambazo zimesajiliwa zinatoa mikopo kausha damu kama taasisi nyingine ambazo hazijasajiliwa.

"Naibu Waziri wa Fedha nakupa muda baada ya kipindi cha maswali katafute habari za uhakika hapo nje kwa kampuni za simu kama zinatoa mikopo kausha damu,"alisema.

Awali, akijibu maswali ya wabunge hayo, Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, alielekeza taasisi zinazotoa mikopo hiyo kuacha mara moja na serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu suala hilo.

Pia aliagiza BOT kufuatilia taasisi zinazoenda kinyume na sheria hiyo, na serikali haitakuwa na muhari kwa taasisi zinazokiuka sheria hizo na kanuni hizo , ikiwamo ya kufutiwa leseni ya kutoa huduma hiyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jitihada zaidi zinahitajika mapambano dhidi ya malaria

**LEO** ni Siku ya Malaria Duniani ambayo imekuwa ikiadhimishwa kila mwaka tangu ilipoanzishwa na nchi wanachama wa Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 2007 wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Afya.

Lengo la kuadhimisha siku hii ni kuweka msisitizo katika mapambano ya ugonjwa huu hatari ambao umegharimu mamilioni ya watu duniani. Mapambano hayo dhidi ya malaria ni kuonyesha umuhimu wa uwekezaji endelevu na utashi wa kisiasa katika kukinga na kudhibiti malaria.

Kaulimbiu ya mwaka huu katika kuadhimisha siku ni "Kuongeza Nguvu Katika Mapambano Dhidi ya Malaria" ikisisitiza jitihada za pamoja kwa mataifa yote duniani katika kuzuia, kupambana na kutokomeza malaria. Kwa Tanzania, maadhimisho yatafanyika katika viwanja vya Shule ya Sekondari Uyui, Tabora na mgeni rasmi atakuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

Wakati maadhimisho hayo yanafanyika pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanyika kwa serikali kushirikiana na wadau wa maendeleo pamoja na sekta binafsi, takwimu zinaonyesha kuwa bado ni hatari hasa kwa watoto wachanga na walio chini ya miaka mitano pamoja na wajawazito. Aidha, nchi za Afrika ikiwamo Tanzania, kwa mujibu wa takwimu, ndizo zinazoathirika zaidi na malaria hivyo jitihada zaidi zinatakiwa katika kupambana na kutokomeza maradhi haya.

Tamwinu za WHO zinabainisha kwamba mwaka 2022, kulikuwa na vifo 608 000 vilivyotokana na malaria na maambukizi mapya ya ugonjwa huo yalikuwa milioni 249. Asilimia 94 ya vifo na maambukizi hayo ilikuwa katika bara la Afrika na kwa mantiki hiyo, jitihada zaidi zinapaswa kufanywa kwa Afrika katika mapambano dhidi ya malaria.

Kutokana na ukweli huo, nchi za Afrika kupitia jumuia za kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Uchumi kwa nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU) zinapaswa kuweka moja ya ajenda za kipaumbele kwenye mikutano yao.

Nchi hizo, ambazo ndizo waathirika wakubwa wa malaria, kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo na mashirika ya kimataifa zinapaswa pia kuweka mikakati thabiti katika kupambana na malaria ili kunusuru nguvu kazi na kuzifanya nchi ziwe na ustawi.

Kuna kampeni mbalimbali na mikakati ambayo imefanyika katika kupambana na malaria katika ngazi mbalimbali lakini bado tatizo ni kubwa, hivyo inahitajika mikakati zaidi katika vita hivyo. Ili kufanikisha hilo, mapambano yanapaswa kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa na si kuachia wataalamu pekee.

Katika kufanya hivyo, kila Mtanzania anapaswa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya yakiwamo kuteketeza mazalia ya mbu katika maeneo ya makazi, kutumia chandarua chenye dawa, kuwakinga watoto wachanga na walio chini ya miaka mitano pamoja na wajawazito ambao ndio walio katika hatari zaidi ya kupatwa na ugonjwa huo.

Aidha, imekuwa ikisisitizwa kuwa mtu anapoona dalili za malaria, hana budi kufika katika kituo cha kutolea huduma za afya kwa ajili ya vipimo na atakapobainika apatiwe matibabu stahiki.

Licha ya maelekezo hayo, idadi kubwa ya Watanzania hawazingatii ndiyo maana ugonjwa huo umekuwa ukizidi kugharimu maisha ya watu huku taifa likiendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kinga na tiba.

Ni dhahiri kwamba iwapo kila mtu atazingatia maelekezo ya wataalamu wa afya katika kujikinga na malaria, kutakuwa na mafanikio makubwa katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo na hatimaye kuwa na Tanzania isiyo na maambukizi wala vifo vitokanavyo na malaria.

Shime kila Mtanzania asimame katika nafasi yake huku akisema Tanzania, Afrika na dunia bila malaria inawezekana. Hapo ndipo ushindi dhidi ya maradhi haya utakapopatikana na hatimaye maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi kuonekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Inahitajika elimu endelevu umma upate utamaduni wa kudai risiti

**NI** ukweli usiopingika kuwa Watanzania wengi hawana utamaduni wa kudai risiti wanaponunua bidhaa.

Wanunue TV, redio, nguo, cherehani, akishatoa pesa ataondoka tu. Atasuburi kama kuna chenji imebaki, ni mara chache sana kusikia anadai risiti.

Nimesona habari moja kutoka jijini Mbeya juu ya Maofisa wa Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA), walipofanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka na masoko jijini Mbeya, kuangalia namna ya wafanyabiashara wanavyotekeleza sheria za nchi, walichokutana nacho ni kwamba wananchi wengi hawana habari kabisa kuchukua risiti.

Mmoja wa wafanyabiashara, akasema baadhi ya wananchi huwa wananunua bidhaa na kuondoka nazo bila kuchukua risiti, hata kama watakumbushwa, jambo ambalo alisema linahitaji elimu.

Akasema, unapowauliza kwa nini huwa hawazitaki, hujibu kuwa hazina maana kwao zaidi ya bidhaa walizonunua.

"Kwa mfano, hapa kuna dada mmoja amekuja kununua chombo, lakini nilipompa risiti akaikataa, akidai eti ni uchafuzi wa mazingira na kuondoka, sasa jambo hili linatugombanisha na serikali," alisema mfanyabiashara huyo.

Ukiangalia ni kweli kabisa, wakati mwingine wafanyabiashara wanaonewa kuonekana kama vile wao ndiyo hawawapi risiti wanunuzi.

Ingawa ni kweli wapo baadhi ya wafanyabiashara wana tabia hiyo kwa sababu zao binafsi, lakini siyo Mbeya tu, Watanzania wengi hawana utamaduni wa kuchukua risiti wanaponunua chochote kile.

Huwa wanakumbuka tu pale wanapokamatwa na kukutana na kibano cha TRA, ndipo watakaporejea kwenye duka ambalo amenunua.

Hii inatokana na utamaduni, tabia ya malezi ya huko nyuma.

Mambo ya risiti kusema kweli yaliletwa na Wakoloni na mifumo iliyoko ya maendeleo, lakini kiasili Waafrika hawakuwa na tabia hiyo.

Na hata baada ya Uhuru, bado hakukuwapo mikakati, au serikali zilizopita zilikuwa na mambo mengi ya kufanya na hazikuweka kipaumbele sana katika masuala hayo ambayo waliona yatakuja kuwachanganya tu wananchi wake.

Wakatilia mkazo kwenye elimu, afya, uchumi na vingine vinavyofanana na hivyo. Ndiyo maana unaona hata kwenye mirathi, mtu kutunza nyaraka inakuwa tabu.

Kwa sasa nchi zetu zimeendelea, na kutokana na mazingira ya sasa ya kiteknolojia risiti zina umuhimu sana.

Pamoja na hayo, bado wananchi wana dhana zile zile za kizamani, hivyo serikali inatakiwa kwanza ijikite kutoa elimu taratibu.

Iwekeze huko, ili kila mwananchi ajue umuhimu wa kuwa na risiti kwa kitu chochote kile anachonunua.

Ukitaka kujua watu hawajui umuhimu, inaweza kuibiwa TV huko, polisi watamkamata mtu ambaye anayo kama iliyoibwa, lakini kwa sababu hana risiti, akachukuliwa kudhaniwa kuwa mtuhumiwa, lakini siyo.

Kumbe tu masikini ya Mungu, alinunua na kuacha risiti dukani, ambayo ingemuokoa kukamatwa na polisi kushukiwa ni mwizi.

Ni ukweli usiopingika kuwa pamoja na kusoma, lakini bado watu wengi hawajaelimika, hata msomi anaweza kuacha risiti, hivyo bado serikali kupitia TRA, ina dhima ya kutoa mafunzo.

Inaweza kuweka matangazo, mikutano, pamoja tuzo na zawadi kwa watu ambao wanaotunza risiti kwa kila wanachonunua.

Hii inaweza kuwaamsha wengine wakaanza kudai risiti kwa sababu wanajua kuna zawadi zinazotolewa na baada ya hapo kila mmoja akili inaanza kumuingia ya kuona kumbe zina umuhimu.

Na hapo serikali itakuwa imepiga ndege wawili kwa jiwe moja, wananchi wanapata elimu, yenyewe ikipata mapato yake inayoyahitaji kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

HABARI KITAIFA

# NFRA yanunua tani milioni 294 za chakula

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), imenunua na kuhifadhi tani 294,069.216 kwa ajili ya kusambazwa katika maeneo ambayo yatabainika kuwa na upungufu wa chakula, Bunge limeelezwa.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kalenga (CCM), Jackson Kiswaga, ambaye alihoji serikali imejipangaje kukabiliana na tatizo la njaa linalosababishwa na upungufu wa mvua.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Silinde alisema nchi imekuwa ikijitosheleza kwa chakula kwa kigezo cha upimaji wa utoshelevu kati ya asilimia 112 na 126 kwa kipindi cha miaka 10 mfululizo.

Pia alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha upungufu wa mvua na kuhatarisha usalama wa chakula, serikali imechukua hatua kadhaa.

Alitaja hatua hizo ni kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kutoka hekta 727,280 msimu wa 2022/23 hadi kufikia hekta 1,200,000 ifikapo 2025.

"Hatua zingine ni kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mazao zinazohimili mabadiliko ya tabianchi na usambazaji wa mbolea kwa mpango wa ruzuku na kuimarisha miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya chakula kupitia NFRA kutoka tani 360,000 hadi tani 500,000 ifikapo 2025,"alisema.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Grace Tendega, alihoji serikali ina mkakati gani wa kudhibiti utaratibu wa wafanyabiashara wanaotoka nje ya nchi kununua mazao nchini kwa fedha taslimu.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema serikali ilitoa tangazo kwa umma Mei 23, 2023 na kuweka utaratibu wa kufuata ili kudhibiti ununuzi holela wa mazao ya kilimo kutoka kwa wanunuzi wanaotoka nje ya nchi.

Silinde alisema utaratibu huo umefafanua hatua za kufuata kwa manunuzi wa mazao kutoka nje ya nchi ikiwamo kununua mazao kupitia mifumo rasmi ya kifedha.

Alisema katika kudhibiti ununuzi holela wa mazao ya kilimo, serikali inaendelea na uandaaji wa kanuni kwa mujibu wa sheria ya usalama wa chakula sura 249 na marekebisho yake ya mwaka 2009 kupitia sheria ya nafaka na mazao mchanganyiko.

"Kupitia kanuni hizo, serikali itaandaa mwongozo kuhusu utaratibu wa uuzaji na ununuzi wa mazao ikiwamo kununua kwenye masoko ya upili pamoja na kusajili wanunuzi wa mazao wa ndani na nje ya nchi," alisema. Pia alisema lengo ni kuwatambua, kuwasimamia na kufuatilia shughuli zao kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa.



Ofisa Ardhi Mteule wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Selestin Liweje (wa pili kulia), akitoa ufafanuzi kuhusu masuala ya ardhi kwa Shekhe wa wilaya hiyo, Abdallah Seif wakati wa kliniki maalumu ya kutatua kero za migogoro ya ardhi papo kwa papo, katika viwanja vya stendi ya Bombani, jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Nyumba kijiji cha wavuvi zabomoka

**Na Romana Mallya**

WANANCHI wa Kijiji cha Wavuvi, Mtoni Chaurembo, Temeke mkoani Dar es Salaam, wako hatarini baada ya baadhi ya nyumba zao kusombwa na maji kutokana na sehemu ya mtaro uliojengwa maeneo hayo kubomoka.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hii juzi, baadhi ya wananchi hao walisema tatizo hilo limechangiwa na namna mtaro huo ulivyojengwa.

Amani Mpakasini, mmoja wa wakazi wa eneo hilo, alisema shida iliyoko kuna Barabara za Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) zilizojengwa ndani ya mitaa ambako maji ya mitaro yake imeelekezewa baharini waliko wao.

"Njia ya kwanza ya maji waliiacha wakatengenezea njia sehemu nyingine, lakini shida inayokuja ni kule maji yanakoelekea baharini. Mtaro umetengenezwa kwa zege wameweka kama milimita nane tu kisha wakajengea matofali ambayo yamesomwa na maji.

"Hali hii imesababisha maji kuathiri nyumba zilizoko eneo hili. Nyumba moja imedondoka yote na nyingine kibaraza kimeondoka na pia, kuna yadi imeathiriwa. Kama hakutathibitiwa mapema maana yake athari itakuwa kubwa zaidi," alisema.

Alisema mkandarasi aliyejenga mtaro huo huku unakomalizikia ili maji yaende baharini ndiko kwenye shida kwa kuwa maji ni mengi yanayosababishwa na mvua inayoendelea kunyesha.

"Walikuja mbunge na diwani walituambia imetengwa Sh. milioni 11 lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea. Ujenzi huu haujamaliza hata mwaka. Una miezi saba kama sikosei," alisema mwananchi huyo.

Mpakasini aliomba serikali kuangalia uwezekano wa kuukarabati mtaro huo haraka ili kupunguza athari kwao kwa kuwa, mvua zinazoendelea kunyesha zinasababisha maeneo hayo kuliwa na maji na udongo kumeguka kuelekea katika makazi.

Moja wa wafanyakazi wa yadi iliyoathiriwa na maji ya mtaro huo, ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alisema mtaro huo ulijengwa, ili kukusanya maji maeneo mbalimbali na kuyapeleka baharini.

"Kila siku tatizo linaongezeka. Shida kubwa ni waliotengeneza mtaro huu yawezekana kuna mahali walikosea unavunjika tu.

"Hili eneo kuna bahari kwa hivyo maji yanachimba na tayari kumetengeneza shimo ambalo linatokana na maji ya mtaro huu," alisema.


Kamal

**KAMAL GASES LIMITED**

**TAARIFA KWA UMMA**

Sisi **Kamal Gases limited** wazalishaji namba moja wa gesi za viwandani zenye ubora uliothibitika na Shirika la viwango Tanzania TBS.

Tumegundua kuwepo kwa wazalishaji wa gesi wanaotumia mitungi yenye nembo ya KGL kinyume na sheria.

Tunawatangazia wazalishaji, watumiaji wa gesi za viwandani na umma kwa ujumla kwamba ni kinyume cha sheria kujaza, kuuza, na kusambaza gesi iliyowekwa kwenye mitungu yenye nembo ya kamal ambayo haikuzalishwa na Kamal Gases Limited.

Hivyo mnahabarishwa kwamba; Kamal Gases Limited wapo katika zoezi kabambe la kufuatilia na kukamata wahusika wote wanaozalisha gesi za viwandani na kujaza katika mitungi yenye nembo au alama ya kamal gases limited kinyume cha utaratibu.

Kamal Gases Limited itachukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufungua kesi za madai na jinai kwa yoyote atakaye tumia mitungi ya gesi yenye nembo ya Kamal Gases Limited kujaza gesi aliyoichakata mwenyewe au iliyochakatwa na wazalishaji wengine nje ya Kamal Gases Limited

Tunatoa wito kwa wateja wetu kuendelea kutumia huduma ya gesi ya Kamal Gases Limited kwa kupitia vituo vilivyoidhinishwa na kuitambulika na Kamal Gases Limited au wafike kiwandani chang'ombe industrial area plot no. 188/2 kwa maelezo zaidi piga simu namba **+255 765 169 444**

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Kamal Gases Limited**
**Dar es Salaam**

BancABC part of atlasmara

# AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 31-Mar-24 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31-Dec-23 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,627 | 4,045 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 21,738 | 14,064 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 42,067 | 41,323 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 5,238 | 6,123 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 281 | 171 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 92,783 | 87,183 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 133,251 | 130,858 |
| | | | - |
| 12 | Mali Nyingine | 13,991 | 12,525 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,519 | 1,519 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,508 | 2,872 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **318,003** | **300,683** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 30,209 | 25,515 |
| 18 | Amana za Wateja | 158,171 | 147,064 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,753 | 4,745 |
| 28 | Madeni | 117,256 | 114,519 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **309,390** | **291,843** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **8,613** | **8,840** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 139,306 | 139,306 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 200 | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (133,915) | (120,720) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (210) | (12,979) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,233 | 3,233 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **8,613** | **8,840** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 9,936 | 1,945 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,364 | 6,162 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 5,155 | 4,815 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 2.71% | 2.94% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.60% | 4.50% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 73.47% | 76.63% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 41.90% | 43.98% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 44.84% | 45.79% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 9.16% | 5.84% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 5.76% | -5.26% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Mar-24 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 31-Mar-23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-24 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Mar-23 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,729 | 10,283 | 10,729 | 10,283 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,908) | (4,919) | (4,908) | (4,919) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,821** | **5,364** | **5,821** | **5,364** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 278 | - | 278 | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (142) | - | (142) | - |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,212** | **1,267** | **1,212** | **1,267** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 542 | 519 | 542 | 519 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 342 | 298 | 342 | 298 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 328 | 450 | 328 | 450 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(7,327)** | **(7,711)** | **(7,327)** | **(7,711)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,868) | (2,695) | (2,868) | (2,695) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (4,459) | (5,016) | (4,459) | (5,016) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(158)** | **(1,080)** | **(158)** | **(1,080)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (53) | (59) | (53) | (59) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(210)** | **(1,138)** | **(210)** | **(1,138)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(210)** | **(1,138)** | **(210)** | **(1,138)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 168 | 172 | 168 | 172 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.09) | (0.46) | (0.02) | (0) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 6 | 6 | 6 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.27% | -1.44% | -0.27% | -1.44% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -9.65% | -23.79% | -9.65% | -23.79% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 104.18% | 116.28% | 104.18% | 116.28% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.24% | 3.05% | 3.24% | 3.05% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Mar-24 | Robo Mwaka iliyopita 31-Dec-23 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (158) | (12,744) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 698 | 4,665 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,252) | (7,919) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 15,801 | (36,216) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (744) | 2,633 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (992) | 516 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 6,663 | 4,943 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (53) | (235) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **18,964** | **(44,357)** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (376) | (5,051) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | 14,354 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(376)** | **9,303** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | (2,570) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | 16,352 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 2,737 | 15,431 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **2,737** | **29,213** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 21,326 | (5,841) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 103,060 | 108,902 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **124,386** | **103,060** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2024
(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **139,306** | **-** | **(133,699)** | **-** | **-** | **3,233** | **8,840** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (210) | - | - | - | **(210)** |
| Hisa za upendeleo | - | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (200) | 200 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **139,306** | **-** | **(134,125)** | **200** | **-** | **3,233** | **8,613** |
| | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(120,720)** | **-** | **-** | **3,018** | **5,252** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (12,979) | - | - | - | **(12,979)** |
| Hisa za upendeleo | 16,352 | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | 215 | **215** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **139,306** | **-** | **(133,699)** | **-** | **-** | **3,233** | **8,840** |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 25-Apr-24 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 25-Apr-24 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 25-Apr-24 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 25-Apr-24 |
| 2 Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 25-Apr-24 |



# Majaliwa atoboa siri kufufua viwanda Tanga

**Na Hamida kachalla,** TANGA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema serikali imefufua viwanda vingi katika Mkoa wa Tanga vikiwemo vya kuchakata zao la mkonge ikiwa ni jitihada za kuvirejesha na kuwezeshwa kuingia kwenye uchumi wa viwanda.

Majaliwa alitoa kauli hiyo wakati akiweka jiwe la msingi kwenye mradi wa jengo la kitega uchumi la Halmashauri ya Jiji la Tanga ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano wa Tanzania yatakayofanyika kesho. "Tumefufua viwanda vingi vya mkonge, zao ambalo lilikufa kabisa katika wilaya zote mkoani hapa, sasa serikali ya awamu ya sita imekusudia kuvifufua ili kuingia kwenye uchumi wa viwanda, " alisema.

Aliwataka wakazi wa Tanga kuchangamkia fursa za uchumi wa buluu kutokana na mkoa huo kuwa na uwezo mkubwa wa kusafirisha shehena zinazotokana na bahari.

Majaliwa, alisema idadi ya wavuvi ni ndogo ikilinganishwa na eneo la bahari, hivyo hakuna sababu ya kuacha kutumia fursa hizo na kutumia bahari hiyo vizuri.

"Serikali yenu imeamua kujenga bandari kubwa ya uvuvi wilayani Kilwa (Mkoa wa Lindi) kwa sababu bahari ile pamoja na bahari kuu inatoa samaki maarufu Duniani anayeitwa 'Tuna' na ana bei kubwa, kwa hiyo kwa kuweka bandari ile tulikuwa tunashawishi pia wawekezaji wenye meli zinazovua bahari kuu waje wavue," alisema.

Alifafanua kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliondolewa kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuipa wepesi wa kuratibu shuhuli zake pasipo muingiliano.

"Na mimi sina shaka wote mnafahamu manufaa ya uvuvi sababu mko karibu na bahari, kiwango cha ulaji wa samaki nchini kimepungua, lakini siyo kweli samaki wamepungua baharini bali wajasiriamali wanaotaka kujikita kwenye uvuvi ndiyo wamepungua, samaki tunao lakinu tunashindwa kwenda kuvua," alisema Waziri Mkuu.

Kufuatia hali hiyo, alisema katika kipindi cha miaka mitatu, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amenunua boti za kisasa za kuvulia 222 na kuanza kuzigawa mikoa ya Kanda ya Ziwa, ikifuatiwa na ya Pwani, Tanga, Dar es Salaam na Lindi ili wajasiriamali wote wapate na kuzitumia kujiingizia kipato.

Majaliwa aliwaagiza wakuu wa wilaya zote zilizopo mwambao wa bahari hiyo kuwahamasisha wananchi wavuvi kujikita katika uvuvi na kutumia fursa kupitia uchumi wa bluu.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Buriani, alisema mkoa huo wa kimkakati hususani kupitia zao la mkonge, hivyo serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kuendeleza kilimovili ni kukuza uchumi.

"Kama tunavyojua mkoa wetu unaenda kupanuka kiuchumi kutokana na maboresho makubwa yaliyofanywa na Rais wetu, tuendelee kuimarisha uchumi kupitia zao la Mkonge na viungo ikiwa ni pamoja na kutumia fursa za uchumi wa buluu ili kufungua uchumi," alisema Batilida.

Akitoa salamu za chama, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Mkoa huo, Rajab Abdallah, alisema wananchi mkoani humo wana amani ambayo inalindwa na serikali yao.

"Thamani ya amani katika nchi yetu ni kubwa sana na sisi Wanatanga tumejipanga vya kutosha kuhakikisha kwenye Uchaguzi Mkuu mwaka 2025 Tanga tutaongoza kwa kura za Rais nchi nzima,

"Hii ni kutokana na maendeleo makubwa yanayofanyika katika uwekezaji mkubwa wa fedha za serikali kwenye mambo mbalimbali ya kimandeleo, tunayo sababu ya kuendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya," alisema Abdallah.

# Wabobezi wa sheria Afrika wapiga kambi Arusha

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WABOBEZA wa sheria wa mataifa ya Afrika wapo jijini hapa kwa siku saba kujadili njia bora za kutatua migogoro kwenye bahari na maziwa makuu kwanchi zao.

Vilevile, watashiriki mkutano wa sheria ya mipaka kwenye maeneo ya bahari wa siku saba ukiwa na lengo la kuwapatia mafunzo washiriki na kujengewa uwezo.

Akizungumza jana jijini hapa wakati akifungua mkutano huo, Charles Mtae, Mwanasheria kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, alisema mkutano huo utawajengea uwezo wataalamu hasa inapotokea mgogoro wa mipaka ya bahari.

Mtae,alisemamkutano utawasaidia washiriki kutoka mataifa hayo kuzifahamu vema sheria za mipaka ya bahari kwa kuwa kuna wataalamu wabobezi wa muda mrefu wa utatuzi wa migogoro hiyo.

"Uwepo wa wataalamu hao hapa itawasaidia washiriki kuongeza ujuzi na maarifa ya kufahamu sheria na utararibu kuhusu utanuzi na uongezaji wa mipaka ya bahari katika nchi husika," alisema.

Mkurugezi wa Taasisi ya African Institute Of International Law, Profesa Mathias Sahinkuye, alisema taasisi hiyo ilipewa jukumu la kuandaa mkutano huo ambao utawakutanisha washiriki zaidi ya 50 kutoka katika mataifa hayo.

"Asilimia 90 ya washiriki wanatoka katika nchi za Afrika, lakini wakufunzi wa wafunzo wengi wao wanatoka nje ya bara bara hilo ikiwamo nchi ya Hispania, Island, Denmark na Oman.

"Mkutano huu ni mkubwa na tutajikita zaidi kujadili sheria za bahari kwa kuwa ni sehemu ya utekelezaji wa mipango ya taasisi yetu ikiwamo kukuza na kutangaza utawala bora wa sheria kwa nchi za Afrika," alisema Prof. Sahinkuye.

Alisema wananchi wengi hawafahamu sheria za mipaka ya bahari na wakati mwingine wamejikuta wakisababisha migogoro kati ya nchi na nchi pasipo kufahamu hivyo watatumia fursa ya mkutano kuwaongezea ujuzi wataalamu hao ili wakatoe elimu kwenye maeneo yao.

Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Khadija Shamte, alisema mkutano huo utakuwa na manufaa kwa Tanzania na Zanzibar ikiwa ni pamoja na kutunga sera nzuri na sheria za usuluhishi wa migogoro hiyo.

BancABC part of atlasmara

AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **IZZE** | | | |
| Account Opening Fee | Free | NA | NA |
| Opening balance | Free | NA | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NA | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 10,000.00 | NA | NA |
| Monthly Service Fee | Free | NA | NA |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 5,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 100,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| **CURRENT ACCOUNT** | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 50,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| **SME TIERED CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | NA |
| **JAMII CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | Free | Free | Free |
| Minimum Operating Balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 50,000.00 | £ 50,000.00 |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | Free |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 1.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE TIERED INTEREST ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000,000.00 | $ 100,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | NA |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| Technical | TZS 30,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 20.00 |
| 100 leaves | TZS 50,000.00 | $ 35.00 | £ 35.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 1% Per Cheque + $20 | 1% Per Cheque +$20 |
| Stop Payment Charges | TZS 30,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | Free | Free | Free |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | Free | Free | Free |
| Standing Order - Other local bank | TZS 20,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Amendment | Free | Free | Free |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 5% Min 10,000 | NA | NA |
| Cash Deposit at Branch small denominations less than 50USD (USD 1,2,5,10,20) equal and above USD 500 | NA | 3% of FCY currency value | 3% of FCY currency value |
| With Account Transfers (Internal) | Free | Free | Free |
| Cheque deposit | Free | Free | Free |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to 2m | TZS 3,500.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 2m to 20m | TZS 4,000.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) above 20m | 0.15% Max 50,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3,000 Max 20,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 3,000 Max 100,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 3%On small denominations above $500 | 3%On small denominations above $500 |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | NIL | NIL | NIL |
| Dormant Account monthly fee | NIL | NIL | NIL |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 2,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Reference Letter | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 11,800.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,500.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | $50 + Other overseas bank chrges | $50 + Other overseas bank chrges |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 |

AGENCY BANKING FEE

| | |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Bill payment | Free |

Withdrawal Fees

| Transaction tiers | BancABC Fees | Government Levy | Total Fees |
|---|---|---|---|
| 0-999 | N/A | - | N/A |
| 1,000-1,999 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000-2,999 | 300 | 11 | 311 |
| 3,000-3,999 | 300 | 19 | 319 |
| 4,000-4,999 | 300 | 39 | 339 |
| 5,000-6,999 | 500 | 70 | 570 |
| 7,000-9,999 | 500 | 88 | 588 |
| 10,000-14,999 | 600 | 224 | 824 |
| 15,000-19,999 | 600 | 427 | 1,027 |
| 20,000-29,999 | 600 | 672 | 1,272 |
| 30,000-39,999 | 700 | 770 | 1,470 |
| 40,000-49,999 | 800 | 1,050 | 1,850 |
| 50,000-99,999 | 900 | 1,435 | 2,335 |
| 100,000-199,999 | 1,000 | 1,771 | 2,771 |
| 200,000-299,999 | 1,100 | 2,058 | 3,158 |
| 300,000-399,999 | 1,200 | 2,450 | 3,650 |
| 400,000-499,999 | 1,200 | 2,870 | 4,070 |
| 500,000-599,999 | 2,000 | 3,640 | 5,640 |
| 600,000-699,999 | 2,000 | 4,480 | 6,480 |
| 700,000-799,999 | 2,000 | 4,970 | 6,970 |
| 800,000-899,999 | 2,000 | 5,264 | 7,264 |
| 900,000-1,000,000 | 2,000 | 6,230 | 8,230 |
| 1,000,001-2,000,000 | 2,300 | 6,580 | 8,880 |
| 2,000,001-3,000,000 | 2,500 | 6,580 | 9,080 |
| 3,000,001 na zaidi | N/A | 7,000 | N/A |





# Makahaba wapeleka kilio cha njaa Shy

## - Wavamia vijijini msimu wa mavuno, wahongwa mpunga

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

BAADHI ya wakazi wa Kata ya Mwamala Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga mkoani hapa, wameiomba serikali kuzinusuru familia zao kufa kwa njaa kutokana na waume zao kuhonga makahaba magunia ya mpunga katika kipindi cha mavuno na kusababisha wao na watoto kukosa chakula.

Mkazi wa Kijiji cha Mwamala 'B', Salima Sosoma alitoa ombi hilo juzi wakati akizungumza na NIPASHE katika utekelezaji wa mradi wa wanajamii na vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto unaofadhiliwa na Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Salima, alisema katika maeneo ya vijijini kuna idadi kubwa ya wanawake kutoka mjini wanaojifanya wanauza vileo huku wakiwa wanauza miili yao kwa ujira wa kubadilisha kuanzia debe moja la mpunga hadi gunia kwa vijana na waume zao hali inayosababisha familia zao kukosa chakula.

"Kama unavyojua sie wanawake wa Kisukuma hatuna sauti mbele za wanaume zetu na ukijifanya mjuaji unaadhibiwa mbele ya watoto, tunaiomba serikali iingilie kati na kuwaondoa madada poa ambao wengi wao wanafukuzwa mjini na kukimbilia vijijini kutapeli mazao yao," alidai.. Ester Kenedy, alisema wanaendelea na uvunaji wa mazao mchanganyiko, ikiwemo mpunga na inapofika nyakati za usiku eneo la katikati ya kata hiyo ambako kuna mzunguko mkubwa wa biashara utakuta madada hao wamejaa kwenye kumbi za starehe ikiwemo zinazouza vileo.

Alisema wanaiomba serikali kuingilia kati na kuwanusuru na janga la njaa ambalo linaweza kutokea baada ya waume zao kujiingiza kwenye ukahaba kwa kuwalipa mazao hayo badala ya fedha.

Alisema wamekuwa wakiona kwenye vyombo mbalimbali vya habari namna serikali inavyowaondoa mitaani makahaba hao na kuwanusuru vijana na kuvunjika kwa ndoa.

" Mbinu inayotumia kuwaondoa makahaba mjini basi itumike pia kuwaondoa vijijini na itasaidia kupunguza maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi katika ndoa na baadhi ya vijana," alidai.

Ofisa Kilimo wa Kata hiyo, West Mwanda alithibitisha baada ya chakula kuisha kwenye familia wanaoteseka ni wanawake na watoto.

Mwanda, alisema amekuwa akikemea tabia hiyo mara kwa mara hasa anapowatembelea wakulima kuwaelimisha kilimo cha kisasa cha mazao ya chakula na biashara.

Alisema hali ya chakula katika kata hiyo ni ya wastani kwa sababu wanazingatia elimu wanayotoa kila wakati na mpunga na mahindi yanazalishwa zaidi.

Aliwataka wakulima kuacha tabia ya kuwapa mpunga wanawake wanaouza miili yao na wale wanaouza kwa lengo la kujipatia fedha kwa ajili ya familia zao wauze kichache na kuacha kingine kwa matumizi ya nyumbani.

Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Suzana Kayenge alisema kwa kulitambua hilo, wameweka utaratibu wa kupima VVU na Ukimwi kwa vijana wanaotaka kuoa na kuolewa lengo la kudhibiti maambukizi yasiendelee kuongezeka katika jamii na vifo kwa kundi hilo.

Susana, alisema anatarajia kuanzisha msako kwa kushirikiana na Kamati za Mtakuwwa na serikali za vijiji na kuonya kuwa watakaobainika hawana makazi wataondolewa mara moja ili kutokomeza biashara hiyo ya ukahaba.




Kaimu Meneja wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Victor Lule (kulia), akikabidhi msaada wa dola za Kimarekani 10,000 kwa Mwakilishi wa Shirika la Ecopeace Women Initiative, Anastazia Magembe, zilizotolewa na taasisi ya kimataifa ya Nos Vies en Partage (NVeP) iliyoanzishwa na kufadhiliwa na Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Barrick Gold Corporation, Mark Bristow katika hafla iliyofanyika katika mgodi huo, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miundombinu yawaliza Butimba

**Na Remmy Moka**, SAUT

WAKAZI wa Mtaa wa Kanyerere Kata ya Butimba Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza wamesema ukosefu wa miundombinu katika barabara yao umesababisha nyumba zao kukumbwa na mafuriko yanayosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha.

Benedicto Mkwavi, mmoja wa wakazi hao aliliambia NIPASHE kuwa nyumba zao zimekuwa zikikumbwa na mafuriko mara kwa mara kutokana na ubovu wa barabara ya mtaa wao, kukosa mtaro na kusababisha maisha yao kuwa hatarini.

Mkwawavi, alisema wamekuwa wakitumia magunia kunusuru nyumba zao kuharibiwa na kukumbwa na mafuriko.

Aliushukuru uongozi wa Chama cha Democrasia na Maendeleo (CHADEMA) Wilaya ya Nyamagana kwa kuwasaidia kuzibua baadhi ya mitaro, wameiomba serikali kuweka miuondombinu hiyo katika hali ya usafi.

Alisema wamekuwa wakiwasilisha malalamiko yao kwa uongozi wa kata hiyo, lakini imeshindwa kulipatia ufumbuzi tatizo hilo.

Zuwena Mapulu, alisema mvua hizo zimesababisha nyumba zao kuwa hatarini kuanguka, licha ya kuzingira, yamekuwa yakijaa hadi ndani.

Zuwena, alisema baadhi ya watoto wake wanaishi kwa ndugu zake kwa kuhofia mafuriko hayo kuwa yanaweza kuleta madhara kwao.

Viongozi wa CHADEMA wakiongozwa na Mhasibu Baraza la Wanawake (BAWACHA) Mkoa wa Mwanza, Veronica Kunju wakishirikiana kuziba mifereji ya ya barabara hiyo ya mtaa, walisema ubovu wa miuondombinu hiyo unasababisha baadhi ya watumiaji wa barabara kukosa huduma zinazostahili.

Marko Christian Mwenyekiti wa Baraza la Vijana CHADEMA (BAVICHA) Wilaya ya Nyamagana, alisema licha ya barabara ya mtaa huo kutengewa fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami, miuondombinu ni mibovu na kuiomba serikali kulifuatilia suala hilo ili kuwarahisishia huduma ya usafri wananchi.

# Wahamasishwa kutumia gesi waondokane na kuni

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Ziwa imesema serikali ina mpango wa kuondoa kodi katika mitungi ya gesi ya kupikia (LPG) ili wananchi waondokane na matumizi ya kuni na mkaa na kutunza mazingira.

Hayo yalibainishwa na Meneja wa EWURA wa Kanda hiyo, George Mhina wakati akizungumza na NIPASHE kuhusiana na mpango huo na kuwahamasisha wananchi kutumia gesi badala ya kuni na mkaa ili kuboresha afya zao na kudhibiti ukataji miti ovyo.

Aliwata wakazi wa kanda hiyo kuendelea kuhamasika kutumia gesi wakati serikali ikiwa na mpango wa kuondoa kodi kwa kuwa ni rafiki wa mazingira, afya zao na gharama yake ni nafuu ikilinganishwa na kuni na mkaa.

"Pamoja kusisitiza umuhimu wa kutumia nishati ya gesi, tunatoa rai matumizi yake yafanyike kwa usahihi, tunaponunua gesi tuhakikishe tumeipima uzito wa mitungi, usafirishaji wake na haina mivujo," alisema Mhina.

Alisema mamlaka hiyo inaendelea kufuatilia huduma zao katika maeneo ya Kanda ya Ziwa hasa mafuta kwa kupima vinasaba.

Alisema hadi sasa wamepima vituo vya mafuta takriban 82 kwa lengo la kubaini nishati hiyo inayotumiwa kama imelipiwa kodi.

Mhina, alisema walipima ubora wa mafuta katika vituo 62, kati ya hivyo viwili vilibainika mafuta yake hayana ubora unaotakiwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kuvifungia. Akizungumzia sekta ya maji, alisema katika uchunguzi wao wamebaini mamlaka nyingi hazina mifumo ya kuondoa na kutibu maji taka.

"Ni mamlaka chache zina mifumo hiyo ingawa taarifa inaonesha zimeongezeka kutoka 18 kwa ripoti iliyopita, kiwango hicho bado ni kidogo kwani nchi nzima kuna mamlaka 85, hivyo inahitaji uwekezaji zaidi," alisema.

Kwa mujibu wa Mhinda, baadhi ya mamlaka hazina mpango wa biashara nwa kwamba kati ya 85 ni 57 ndio zina mpango huo, hivyo eneo hilo bado lina tatizo.

Alisema kumekuwa na mwitikio wa wadau kujitokeza kutuma maombi ya kutaka kuwekeza katika kujenga vituo vya mafuta vijijini, ikiwemo vya Wilaya ya Ukerewe (Mwanza), Serengeti (Mara) na maeneo mengine ya mikoa ya kanda hiyo.

ama
ALHAMISI APRILI 25, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12


**Dozi moja inavyotosha kufanikisha kuzuia saratani shingo ya kizazi**



Ukurasa 13

ZIMAMOTO & MGAMBO WA UOKOAJI...

Serikali inavyojipanga zama mpya kukabili majanga kwa staili ngeni



Ukurasa 14

**Mradi 'e- Fahamu' unavyowavusha wenye ulemavu kuziona haki na ufanisi darasani**

MAZINGIRA

UNASABA WA SAMIA NA AFYA...

# Amewekeza mabilioni kwa rasilimali afya, akisogelea kufadhili tiba watoto

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA historia ya afya inayosifiwa leo kiserikali Awamu ya Sita, inashika sura kadhaa.

Mwanzo wake una mzizi wa kasi ya upanuzi ulioanzia katika awamu tatu za serikali zilizopita. Ni mwaka 1996, Rais Benjamin Mkapa akapitisha sheria ya kuwa na Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), kuisaidia Hospitali Kuu ya Muhimbili, wakati huo.

Baadaye katika Awamu ya Nne, kukashuhudiwa maboresho yenye sura mbili za awali. Kwanza, serikali ikabuni Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM), ambayo ndio usukani wa yote yanayofanyika sasa, ikitimia miaka 16.

Kila mtaa au kitongoji kuwa na Zahanati, pia Kata kuwa na Kituo cha Afya na wilaya inakuwa na Hospitali. Kuanzia mkoa, Hospitali za kanda, hadi Muhimbili iliyopewa hadhi mpya Hospitali ya Taifa (MNH) zikawa za rufani.

Vilevile, MOI ikiongezewa jukumu la kutibu mishipa ya fahamu, eneo nyeti ambalo pia lilikuwa na mabingwa tiba wa kuhesabu.

Muasisi Rais Jakaya Kikwete, tena akabuni taasisi ya Moyo, JKCI, hali kadhalika ikashuhudiwa katika Awamu ya Tano, uhamisho makao makuu ya nchi kuwa mkoani Dodoma, kukibuniwa hospitali kubwa ya rufani.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu akikagua tiba ya watoto wenye vichwa vikubwa katika Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), Dar es Salaam, siku chache zilizopita, ambako akatangaza ufadhili wa tiba kutoka kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MAKTABA**

Sura ya pili katika maendeleo hayo, ni kusambaza utitiri wa vituo vya afya, zahanati na hospitali kwa mikoa na maeneo yasiyokuwa na hospitali za rufani.

Hapo ndipo panakozaliwa rekodi katika kipindi cha miaka mitatu sasa ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kumejengwa zahanati na vituo vya afya zaidi ya 300, 'kazi ikiendelea' kwa kasi kubwa.

Vilevile kuna la tatu analolitenda, uwekezaji mkubwa wa vifaa na nguvu kazi ya wataalamu, kuanzia ajira na kugharamia masomo hadi ngazi ya shahada ya uzamivu kila mwaka kukuza uwezo wa nchi katika fani hiyo.

Ndani ya stadi hiyo, kuna ukaribishaji stadi na teknolojia ya tiba, hata imefika hatua Tanzania iko juu zaidi ya nchi jirani za Afrika Mashariki, sasa zinafunga safari nchini kujifunza, staili inayotumiwa na wataalamu kama wa MNH, MOI an JKCI, wanaoenda mikoani kusambaza ujuzi huo mikoani.

Mageuzi hayo yakiwa sehemu ya ajenda kuu ya Rais Dk. Samia katika maendeleo ya Watanzania, imefika hatua sekta afya nayo ina utalii, nchi inapata ugeni kunufaika na 'utalii tiba', huku wataalamu wake wakipata ugeni wa nje ya mipaka, nao wakisafiri kama vile nchini Malawi, kwenda kusambaza ujuzi na huduma itokanayo na ustadi wao.

### ZAO LA MAFANIKIO

Moja ya mafanikio hayo sasa Rais Dk. Samia, mbali na kujenga mazingira bora ya kiutawala, amechukua sura nyingine akiwa ni mwekezaji.

Hivi sasa kukiwapo 'kampeni vichwa vikubwa vinatibika' baadhi ya wadau wakijitokeza, kudhamini tiba yao, wiki hii Rais Dk. Samia amejitokeza kudhamini tiba ya watoto 100.

Hadi sasa inajulikana watoto wazaliwao na tatizo la vichwa vikubwa na mgongo wazi, linawakosesha raha wazazi wengi kutokana na kuwa na uwezo mdogo wa kugharamia matibabu ya watoto wao.

Mfano hai, ni ndani ya wiki moja sasa, imekuwa ikiripotiwa kwenye vyombo vya habari vya elektroniki, namna mama mwenye mtoto mwenye shida hiyo, mkazi wa Chanika, Dar es Salaam, akilia kukwama kumtibu mwanawe, kwa kukosa uwezo tiba.

Hiyo ni picha ya wazazi wasiokuwa na uwezo wanavyopoteza watoto wao kwa kukosa fedha za kuwagharamia matibabu yao.

**INAENDELEA UK.12**

AFYA

# Dozi moja inavyotosha kufanikisha kuzuia saratani shingo ya kizazi




Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mwanza, wakiwa katika maadhimisho ya chanjo ya HPV, katika viwanja vya Furahisha. **PICHA: YASMINE PROTACE**

**Na Yasmine Protace**

Ni maadhimisho ya 'dozi ya chanjo ya HPV', inayomkinga mtoto wa kike asipate ugonjwa wa saratani ya mlango wa shingo ya uzazi.

Chanjo hiyo ya HPV inawalenga watoto wenye umri kati ya miaka tisa na 14, ambayo Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema kuwa dozi moja inatosha kumkinga msichana kupata ugonjwa wa Saratani ya Mlango wa Kizazi.

Waziri Ummy anayaongea hayo kwenye uzinduzi wa Maadhimisho ya Dozi moja ya chanjo ya HPV kwa wasichana, akinena ni jukumu la wazazi na walezi kuhakikisha wanawapeleka watoto kupata chanjo hiyo.

Ni hafla iliyofanyika katika Viwanja vya Furahisha Wilayani Ilemela, Mwanza akiwa na ufafanuzi: "Wataalamu wetu ambao wanatoka kwenye Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR).

> **Wametuhakikishia kuwa dozi moja ya chanjo ya HPV inatosha kumkinga msichana kupata saratani ya mlango wa kizazi.**

"Wametuhakikishia kuwa dozi moja ya chanjo ya HPV inatosha kumkinga msichana kupata saratani ya mlango wa kizazi."

Anasema awali dozi zilitolewa mbili, ya pili ikiwa ni miezi sita akipelekewa binti, hata hivyo wengi hawakurudi kumalizia.

Lakini anaeleza mbadala uliopo ni kwamba, hivi sasa anasema wanatoa dozi moja, inayotosha kuwakinga wasichana dhidi ya maambukizi ya saratani ya mlango wa kizazi.

Waziri anaeleza saratani inayoongoza kuwatesa Watanzania ni 'Mlango wa Kizazi' anayosema katika kila wagonjwa100, wako 23 wagonjwa wa Saratani ya Mlango wa Kizazi. Anaorodhesha saratani zinazofuatia kwa ukubwa ni inayohusu: Mfumo wa Chakula, asilimia 11; matiti asilimia 10.4; tezi dume asilimia 8.9

Pia, Waziri anatoa wito kwa wazazi na walezi nchini, kuhakikisha watoto wao wanapata chanjo zote wanazopaswa, ili wanufaike na kinga dhidi ya maradhi yalitotajwa, ikiwamo lengo kubwa la kuwakinga na magonjwa, yakiwamo haya ya saratani pamoja na kuwakinga na vifo vinavyoweza kuzuilika na chanjo.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi akimwakilisha Mkuu wa Mkoa Mwanza, Saidi Mtanda atahakikisha watoto wote wenye umri wa kuanzia miaka tisa hadi 14, wanapata chanjo hiyo ili kufikia malengo.

"Kwa mwaka 2022/23 Mkoa wa Mwanza ulifanikiwa kuchanja watoto zaidi ya laki Mbili sawa na asilimia 107 kati ya walengwa waliotarajiwa kuchanjwa ni laki 191,440 wenye umri chini ya mwaka mmoja, tumefikia malengo na kuyavuka," anasema.

Mkazi wa Jiji la Mwanza Amina Said, anasema kutolewa kwa chanjo hiyo ni moja ya mapambano ya kumkinga mtoto wa kike asipate saratani ya mlango wa kizazi.

Anasema elimu juu ya chanjo hiyo inatakiwa kutolewa mara kwa mara ili jamii iendelee kuelewa umuhimu wa chanjo hiyo.

"Mimi nina mtoto wa kike ana umri wa miaka name,lakini sina elimu yoyote, kuwa anapofikisha miaka tisa anatakiwa kupatiwa chanjo hiyo," anasema.

Anaongeza kuwa, serikali inapambana kuwahakikishia wananchi wake wawe na afya njema, hivyo ana rai elimu iendelee kutolewa kwa jamii, ijue umuhimu wa chanjo.

Aziza Jumanne, mkazi wa Mwanza anaitaja chanjo hiyo kuwa mkombozi kwa wasichana wenye sifa ya kupata chanjo hiyo, akiishauri jamii izingatie jinsi ya kuwasaidia watoto wa kike wasipate ugonjwa huo.

"Kila mzazi ambaye ana mtoto wa kike aliye na sifa za kupata chanjo, awapeleke kupata chanjo hiyo," anasema, kuwa watoto wanapopatiwa chanjo, wananudhurika kwa maradhi hayo.

Anthony Andrew, mkazi wa Maduka Tisa, jijini Mwanza anasema ni wakati wa wazazi na walezi kuachana na mila potofu dhidi ya kuwapo chanjo hizo na kinachotakiwa ni kuisaidia serikali, ili watoto wapate waelewe.

Andrew anakumbusha chanjo inatolewa bure na inabaki jukumu la walezi na wazazi kujitokeza na watoto wao waweze kupatiwa chanjo hiyo.

"Tumekuwa tunasikia kutoka kwa wataalamu wetu wa afya, magonjwa sugu yanayo changia vifo kwa jamii. Katika magonjwa hayo, saratani nayo ipo," anasema, akiwa na ufafanuzi.

Anaongeza kuwa, saratani zote zina changamoto zake, kama mtu atachelewa kupata matibabu kwa wakati anayonafasi kubwa ya kupoteza maisha.

## Amewekeza mabilioni kwa rasilimali afya, akisogelea kufadhili tiba watoto

**INATOKA UK.11**

Tatizo liko namna gani? Picha halisi iko kwa wanaotembelea hospitali kubwa kama Muhimbili-MNH, kinamama wengi wakiwa wamepakata watoto wenye matatizo hayo huku wakiwa na nyuso za kukata tamaa.

Baadhi yao huokoa watoto wao kwa kuomba msaada kutoka kwa wasamaria wema au taasisi zinazotoa msaada wa matibabu hayo.

Sasa, mageuzi hayo ya kiutawala, inakuwa ujumbe kwa kundi hilo, pale Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anatangaza Rais Dk. Samia atagharimia matibabu ya upasuaji kwa watoto hao 100.

Pia, katika sura ya maendeleo ni hadithi ya ukombozi, kwani taifa linavuka mbali kutoka zama ilikuwa kama tatizo lisilotatulika, kuhamia upande linatatulika tena ndani ya mipaka ya nchi.

Vilevile, hilo linafanyika likiacha ujumbe mkubwa kuwapo mwanamama wa kwanza kongoza nchi na wakati huohuo, akisimamia 'umama' wake kutambua na kutatua matatizo ya watoto ndani ya wasifu 'mama na mtoto huwa hawatenganishwi.'

Pia, anayetangaza kuwajibika huko anabaki 'waziri jembe' hasa wa afya nchini, mwanamama mwanasheria, aliyejivika viatu vya afya na vikamtosha.

Ni mara nyingine inamrudishia wasifu waziri mwenye dhamana, kwamba 'Rais hakukosea kumteua kwa nafasi hiyo.'

Mbali na ufadhili, pia kukua stadi za tiba katika eneo hilo na mengine kama ilivyokuwa katika kampeni za kukabili maradhi ya fistula, leo darasa la kukabili uwezekano wa mtoto kuzaliwa na kichwa kikubwa, au kuwaondolea mabinti uwezekano kuwa saratani ya shingo ya kizazi, kampeni iko juu vilivyo.

Wajibu unaosisitizwa, ni wazazi wenye watoto wenye matatizo hayo sasa, wapelekwe hospitalini na kuachana na dhana kuwa wamelogwa na kuishia kwenda kwa waganga, wakipata maelezo ya uongo na mwishowe kuangukia athari mbaya.

Hayo yanafikiwa na Rais Dk. Samia, huku Chama cha Wazazi na Walezi wa Watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi Tanzania (ASBATH), kikimuunga mkono kwa taarifa ya orodha ya watoto 200 wanaohitaji.

Canara Bank (Tanzania) Ltd.
(Together we can build a better life)

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 Machi 2024 | Robo Mwaka iliopita 31 Desemba 2023 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| | 1 Fedha Taslimu | 396.39 | 511.52 |
| | 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 7,082.37 | 9,797.16 |
| | 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 38,183.73 | 38,180.41 |
| | 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 401.75 | 1,117.74 |
| | 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | (13.38) | 22.94 |
| | 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 Bili zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 1,522.40 | 3,517.44 |
| | 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 43,090.28 | 46,772.72 |
| | 12 Mali Nyingine | 1,740.43 | 1,460.08 |
| | 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,087.53 | 824.19 |
| | **16 JUMLA YA MALI** | **93,491.50** | **102,204.21** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| | 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 771.00 | 1,700.00 |
| | 18 Amana za Wateja | 48,532.45 | 56,378.31 |
| | 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 20 Amana Maalumu | - | - |
| | 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| | 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| | 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,480.30 | 2,091.54 |
| | 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| | 27 Dhima Nyingine | 705.93 | 726.76 |
| | 28 Madeni | - | - |
| | **29 JUMLA YA DHIMA** | **51,489.68** | **60,896.62** |
| | **30 MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29*** | **42,001.83** | **41,307.59** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 Akiba ya Mtaji | 230.53 | 261.30 |
| | 33 Mapato Yaliyobakizwa | 8,247.06 | 7,386.41 |
| | 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 694.23 | 829.89 |
| | 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| | 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **42,001.83** | **41,307.59** |
| | 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 4,288.42 | 4,305.11 |
| | 39 Mikopo Chechefu | 410.12 | 349.31 |
| | 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 75.68 | 178.13 |
| | 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 44.93% | 40.42% |
| | (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.95% | 0.74% |
| | (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 87.54% | 80.80% |
| | (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 46.09% | 45.76% |
| | (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 88.99% | 87.66% |
| | (vi) Ongezeko la Amana | -15.11% | -2.43% |
| | (vii) Ongezeko la Mali | -8.52% | -0.93% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 MACHI 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 31 Machi 2024 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 31 Machi 2023 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Machi 2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31 Machi 2023 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 2,398.39 | 2,113.25 | 2,398.39 | 2,113.25 |
| 2 Gharama za Riba | 611.14 | 803.86 | 611.14 | 803.86 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,787.25** | **1,309.39** | **1,787.25** | **1,309.39** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 1.65 | - | 1.65 | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (102.45) | 10.48 | (102.45) | 10.48 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba** | **145.18** | **207.27** | **145.18** | **207.27** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 48.03 | 48.22 | 48.03 | 48.22 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 97.15 | 159.05 | 97.15 | 159.05 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **1,189.00** | **942.77** | **1,189.00** | **942.77** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 480.04 | 422.76 | 480.04 | 422.76 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 3.15 | 5.86 | 3.15 | 5.86 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 705.81 | 514.15 | 705.81 | 514.15 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **844.23** | **563.42** | **844.23** | **563.42** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 150.00 | 285.00 | 150.00 | 285.00 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **694.23** | **278.42** | **694.23** | **278.42** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 26 | 26 | 26 | 26 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 21 | 8 | 21 | 8 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 21 | 8 | 21 | 8 |
| **14 Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.94% | 1.02% | 2.94% | 1.02% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 6.64% | 2.73% | 6.64% | 2.73% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 61.53% | 62.16% | 61.53% | 62.16% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 8.38% | 5.21% | 8.38% | 5.21% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 MACHI 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 31 Machi 2024 | Robo Mwaka iliopita 31 Desemba 2023 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Machi 2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31 Machi 2023 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 694.23 | 69.62 | 694.23 | 278.42 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| Hasara katika mali | 85.05 | 66.40 | 85.05 | 95.97 |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | 3,682.45 | 936.51 | 3,682.45 | (3,382.64) |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Amana | (8,774.87) | (1,449.11) | (8,774.87) | 2,545.86 |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | (494.11) | 929.74 | (494.11) | 313.15 |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | 258.91 | 631.08 | 258.91 | 215.01 |
| Kodi iliyolipwa | (150.00) | (387.87) | (150.00) | (285.00) |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(4,698.34)** | **796.37** | **(4,698.34)** | **(219.23)** |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | - | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | (348.38) | (27.20) | (348.38) | (0.55) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | 6,442.89 | (6,293.93) | 6,442.89 | 5,553.31 |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **6,094.51** | **(6,321.13)** | **6,094.51** | **5,552.75** |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | 0.00 | (135.88) | 0.00 | (82.27) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **0.00** | **(135.88)** | **0.00** | **(82.27)** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 1,396.17 | (5,660.64) | 1,396.17 | 5,251.26 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 10,958.97 | 16,619.61 | 10,958.97 | 12,085.98 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **12,355.14** | **10,958.97** | **12,355.14** | **17,337.24** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 31/03/2024** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **8,216.29** | **261.30** | **-** | **-** | **41,307.59** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 694.23 | - | - | - | **694.23** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 30.77 | (30.77) | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | **-** | **8,941.30** | **230.53** | **-** | **-** | **42,001.83** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2023** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **7,344.16** | **467.69** | **-** | **-** | **40,641.86** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 829.89 | - | - | - | **829.89** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | (164.15) | - | - | - | **(164.15)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 206.39 | (206.39) | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **8,216.29** | **261.30** | **-** | **-** | **41,307.59** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31MACHI 2024**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| ***Jina*** | ***Cheo*** | ***Sahihi*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|---|
| RAJSHEKHAR SOMASHETT | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 24-04-2024 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 24-04-2024 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 24-04-2024 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| ***Jina*** | ***Cheo*** | ***Sahihi*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|---|
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 24-04-2024 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 24-04-2024 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**

AFYA

TEHAMA YAINGIA DARASANI...

# Mradi 'e- Fahamu' unavyowavusha wenye ulemavu kuziona haki na ufanisi darasani

**Na Frank Monyo**

ELIMU kwa wote, humaanisha namna ya kuhakikisha watoto wahitaji wanapata haki zao za elimu, bila kujali tabaka zao. Kuna mfano hai, wanapojumuishwa watoto wenye ulemavu shuleni, ambao wamekuwa wakitengwa kutokana na hali zao.

Hapo kunamaanisha wanapewa fursa sawa ya kwenda shuleni kushirikiana na wenzao, kujifunza na kuendeleza stadi wanazopenda kwa maisha yao ya baadaye.

Ni hali inayojidhihirisha kama ambavyo shule za sekondari kadhaa zinavyotumia maudhui ya kidijitali yanayotolewa na sekta binafsi, zikipigania fursa sawa kwa wote katika elimu, afya na uwezeshaji kiuchumi.

Hatua mojawapo ni pale, taasisi ya Vodacom kupitia tawi lake la CSR, Vodacom Tanzania Foundation, imekuwa ikifanya miradi ya elimu ya kidijitali tangu mwaka 2017.

Ni katika mwaka huo ambao kupitia taasisi yake, ilianzisha tovuti ya kujifunza mtandaoni, inayojulikana kama 'e-Fahamu', inayotoa maudhui ya kujifunzia na kufundishia kidijitali kwa wanafunzi na walimu.

Hivi karibuni, iliweka maabara kamili ya ICT kwenye Shule ya Sekondari ya Buhongwa iliyopo wilaya ya Nyamagana, Mwanza. Kimsingi, ni maabara iliyoanzishwa kama sehemu ya mpango mkubwa wa kuanzisha shule za mfano za 'e-Fahamu' nchini.

Maria Selestine, mwanafunzi mwenye ualbino katika Shule ya Sekondari ya Buhongwa huko Nyamagana, Mwanza, anasimulia: "Nilikuwa napata changamoto kubwa, kwa sababu maktaba yetu haina vitabu vya kutosha na shule ina wanafunzi wengi.

"Sikuweza kugombania vitabu maktaba, lakini sasa kupitia e-Fahamu, naweza kupata chochote mtandaoni na kupata maelezo kuhusu karibu kila kitu."



Mtalaamu akiwaelezea wanafunzi namna ya kuingia kwenye tovuti ya e-Fahamu katika moja ya shule zinazofaidika na mradi huo, unaotekelezwa na Vodacom Tanzania Foundation. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

Upatikanaji wa teknolojia ya kidijitali na mtandao wa intaneti bado ni changamoto katika maeneo mengi ya Tanzania, hasa vijijini. Katika kupunguza pengo hilo la kidijitali, inatajwa ni muhimu kuhakikisha wanafunzi wanapata fursa sawa za kupata rasilimali za elimu na kukuza stadi za kidigitali.

Mwaka huu inatajwa programu hiyo ya e-Fahamu iliwasilisha maudhui kuhusu stadi za kidijitali, ikiwafundisha wanafunzi jinsi ya kutumia mtandao kwa usalama na maadili, pamoja na namna ya kutumia mitandao za utafutaji kama 'Google' kwa ufanisi wanapokuwa mtandaoni.

Mtesigwa Bulenga, nio Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Buhongwa, anafafanua uzoefu wake kuwa"shule hii ina mfumo wa elimu jumuishi ambayo inawakusanya pamoja wanafunzi wote wenye mahitaji maalum. Tunao wanafunzi wengi, kwa hivyo maendeleo haya ya kiteknolojia yanarahisisha mchakato wa kufundisha."

Hiyo 'e-Fahamu' inaangukia utambulisho ni tovuti inayorahisisha upatikanaji maudhui ya kujifunza sana, vilevile kuhudhria katika namna sahihi darasani.

Vilevile, inatajwa walimu wao wananufaika na zana za kufundishi, zinazoboresha uwasilishaji wao wa masomo kutoka kwenye maudhui wanayonuia darasani.

Inatolewa mfano kwamba, e-Fahamu ina chaneli ya maudhui inayomuonesha mwalimu namna ya kujiandaa na somo kabla hajaenda darasani, huku wanafunzi wakitumia maudhui yanayotolewa na chaneli iitwayo het inayotoa maudhui ya masomo ya hisabati na sayansi kwa njia ya kibunifu.

"Hii programu (e-Fahamu) imenifanya niweze kusoma na kuelewa navyojisomea tofauti na hapo awali, nilipokuwa nategemea mkalimani kuelewa walimu walipokuwa wakifundisha darasani," anasema Zanura Rajabu, mwanafunzi mwenye ulemavu wa kusikia katika Shule ya Sekondari Buhongwa.

Namna ya utendaji wa taasisi Vodacom, imekuwa ikiwekeza katika miundombinu, hali kadhalika kuwa mstari wa mbele kuunga mkono elimu zaidi katika maeneo ya teknolijia ya habari na mawasiliano (Tehama) na mambo ya fedha katika shule za umma.

Lengo hapo linatajwa, ni kuhakikisha matumizi hayo ya Tehama yanazingatiwa katiika elimu nchini, ili wanafunzi wanufaike na kufaidika kuunganishwa kimawasiliano katika ulimwengu wa kidigitali. Akizungumzia lengo la programu ya 'e-Fahamu', Zuweina Farah, Mkurugenzi wa Masuala ya Nje na Vodacom Tanzania Foundation, anasema:

"Tukiwa kama kampuni ya teknolojia ya mawasiliano ya simu, tuna wajibu wa kutoa suluhisho la kutumia teknolojia katika elimu kwa kuleta wanafunzi na walimu karibu na maudhui mijini na vijijini."

Zuweina anaongeza kuwa "kwa maslahi ya kufanya kazi kwa pamoja kama sekta binafsi na serikali, tunalenga kuboresha matokeo ya kujifunza nchini. Lengo letu ni kuwasaidia Watanzania katika ulimwengu huu wa kidijitali na elimu ni sekta muhimu kufanikisha hili."

Taasisi hiyo inajitambulisha katika dhamira ya kuboresha maisha ya Watanzania, ikitumia teknolojia ya mawasiliano ya simu.

Hadi sasa juhudi za taasisi hiyo, zinaendana kwa karibu na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs), hasa SDG Namba Nne, inayolenga kuwapo Elimu Bora, pia namba 10 inayolenga Kupunguza Ubaguzi, hapo mradi husika unaelezwa kugusa wenye ulemavu.

## Bahari mpya kuzaliwa Pembe ya Ethiopia, kuigawanya bara Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

SASA Afrika ina ugeni wa kimazingira. Watafiti wanabashiri bahari mpya inaibuka barani Afrika.

Ni mchakato uliodhaniwa ungechukua kati ya miaka milioni tano na 10, lakini utafiti mpya wa kisayansi unaonyesha kuibuka huko kunaweza kutokea kwa kasi zaidi ya ilivyotarajiwa.

Profesa Cynthia Ebinger, ni Mtafiti katika Chuo Kikuu cha Tulane, Marekani ni mwanazuoni wa jiolojia tangu miaka ya 1980, anaeleza "wakati bahari mpya ilipoanza kuibuka ilitarajiwa kuchukua mamilioni ya miaka lakini sasa inaonekana itachukua chini ya hapo."

Msomi huyo ana maaandiko mengi ya kitaalamu aliyoyachapisha katika majarida ya kisayansi na ndiye mtaalamu anayeaminika zaidi katika fani za jiolojia na mazingira duniani.

Mwaka 2023, alichapisha makala 17, zikieleza namna mkondo mpya wa bahari utakavyoibuka katika eneo la Afrika, Ethiopia ambako liko kwenye mipaka ya nchi hiyo, Eritrea na Djibouti.

Wanajiolojia wanasema, bahari hiyo mpya itaonekana hasa katika nchi za Afrika Mashariki na utafiti mbalimbali zimefanyika.

Tafiti zimechambua 'magma' (udongo wa tope) katika ardhi ya Ethiopia, kulikokuwapo mlipuko wa volkano iliyodumu kwa miaka milioni 45.

Wakati bahari mpya inapoibuka, Bara la Afrika linatarajiwa kijiografia kugawanyika pande mbili. Inadhaniwa, itatenganishwa na bahari mpya ndogo itakayoibuka kati yao.

Wataalamu wanaeleza kuwa Bahari ya Shamu inasogea kwa sentimeta 2.5 kila mwaka kutoka ilipo sasa, huku ardhi ya jirani nazo zikisogea kwa nusu sentimita.

Maji mengi ya chumvi yanatajwa yatatoka iliko Bahari ya Shamu na Ghuba ya Aden, ili kuunda bahari mpya kulingana na utafiti huo.

Tetemeko la ardhi lililotokea nchini Ethiopia mwaka 2005, kwamba imeripotiwa katika utafiti uliotoa ushahidi mwingi wa kugawika Bara la Afrika.

Katika eneo la Afar nchini Ethiopia, inasemekana kwa sasa, eneo la kilomita 60 limeachana ikiwa ni ishara ya mgawanyiko huo.

Utafiti uliochapishwa mwaka 2009, ukiongozwa na Atalay Ayele, kutoka Chuo Kikuu cha Addis Ababa, Ethiopia unaeleza kuwa kugawika kwa bara hilo kumekaribia.

Mwezi uliopita, Ayele na Ebinger, walikuwa sehemu ya kundi la wanasayansi tisa waliochapisha utafiti katika jarida la Tectonophysics.

Miongoni mwa matokeo ya utafiti huo, waligundua 'ukoko mpya ulioibuka kutoka ardhini na safu ya chini ya ardhi ya eneo la Afar ni laini.

**Kwa mujibu wa BBC.**

# Waajiri wasiojisajili OSHA kukiona

Na Augusta Njoji, DODOMA

SERIKALI imesema haitamvumilia mwajiri ambaye hajasajiliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi (OSHA) kwa kuwa anahatarisha afya na usalama wa wafanyakazi kazini.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Deogratius Ndejembi mjini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani kitaifa yatakayofanyika Aprili 28, mwaka huu jijini Arusha.

Ndejembi alisema kuwa Tanzania ina ajali kazini 4,993, magonjwa 249 na vifo 217 kwa mujibu wa takwimu za za Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kuanzia Julai mwaka 2019 hadi Juni 2021.

Alisema pamoja na kuwapo kwa takwimu hizo bado kuna waajiri hawajajisajili ili kuruhusu OSHA kufanya ukaguzi mahali pa kazi. "Wale ambao hawajajisajili wajisajili taarifa zao zitaonekana tu kwa sababu OSHA imeunganishwa na mifumo mtambuka kama ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hivyo watapatikana tu taarifa zao," alisema.

Alisema baada ya maadhimisho hayo, OSHA itaanza kampeni ya kupita kwa waajiri na kwamba serikali haitamvumilia atakayekutwa hajajisajili.

"Na tutakuwa wakali kweli kweli, si tu kwa wale ambao hawajajisajili OSHA, hata ambao wamejisajili, lakini hawajahuisha usajili wao tutapita huko, kwa hiyo Mtendaji Mkuu wa OSHA timu yako pia itembee wale wote ambao tunao kwenye kanzi data," alisema.

Alisisitiza kuwa serikali itaendelea kulinda nguvu kazi ya taifa kwa kusimamia utekelezaji wa sheria namba tano ya afya na usalama mahali pa kazi ya mwaka 2003.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alitaja shughuli zitakazofanyika katika maadhimisho hayo kwa kushirikiana na wadau wa utatu kuwa ni kuendesha kampeni maalum ambayo itatoa mafunzo ya usalama na afya kwa makundi mbalimbali, wakiwamo wajasiriamali wadogo na watu wenye ulemavu. "Kutakuwa na kliniki ya uchunguzi wa afya za wafanyakazi na wananchi. Uchunguzi utahusu magonjwa yasiyoambukiza kama vile kisukari, presha, magonjwa ya moyo pamoja na magonjwa yatokanayo na kazi," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego (wa tatu kushoto) akishiriki zoezi la usafi katika Soko Kuu la Singida mjini juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Serikali yaombwa kuajiri walemavu

Na Peter Mkwavila, DODOMA

SERIKALI imeombwa kutoa asilimia tatu ya ajira ilizotangaza kwa makundi ya watu wenye ulemavu katika sekta ya elimu na afya ili kukabiliana na uhaba wa watumishi nchini.

Hivi karibuni Waziri wa Nchi,Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Geore Simbachawene alitangaza ajira mpya zaidi ya 46,000 kwa watumishi wa sekta ya afya wapatao 12,000 na elimu10,000.

Ombi hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa Karakana ya kutengeneza vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu mkoani hapa, Mwita Marwa wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa baada ya kutangazwa ajira hizo.

Marwa, alisema serikali ikitimiza maelekezo hayo ya kutoa ajira kwa asilimia tatu kwa makundi hayo, itawaondolea adha kupita ofisini na vyeti vyao kuomba kazi.

"Wengi wao wamekuwa wakitembea maofisini na vyeti kwenye mikoba hadi vinachakaa , tunaiomba serikali kwa nafasi hizo wasisaulike," alisema

# Viwanda kuongeza thamani madini kujengwa nchini

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

WADAU wa sekta ya madini wameonyesha nia ya kuanza ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji wa madini ya metali ili kuunga mkono jitihada za serikali kuongeza thamani madini nchini.

Miongoni mwa wadau hao ni Kampuni ya Mineral Access System Limited (MAST) inayotarajia kuanza ujenzi wa viwanda vitatu katika mikoa ya Ruvuma, Dodoma na Lindi mwaka huu kwa gharama ya zaidi Dola za Marekani milioni 15.

Hayo yalibainishwa jana kwenye kikao cha Waziri wa Madini, Anthony Mavunde na wadau hao, Kampuni ya MAST ikiwakilishwa na Mkurugenzi wake, Georgefrey Kente na Mwekezaji kutoka Lithuania, Arunas Sermuksnis, Mkurugenzi wa Kampuni ya Akmenite Limited.

Mkurugenzi Kente, alisema kampuni yake itajenga viwanda hivyo vitatu nchini ili kuongeza thamani kwenye madini.

Mkurugenzi Sermuksnis alihakikishia serikali kuwa wataleta nchini teknolojia ya kisasa ya uchenjuaji wa metali kwa ajili ya kuongeza thamani madini na hatua za awali za uanzishaji kiwanda hicho zimeanza.

Waziri Mavunde alizipongeza kampuni hizo lwa uamuzi huo na kuhimiza ujenzi huo kukamilika haraka ili wachimbaji wa Tanzania wanufaike.

Aliwahakikishia serikali kupitia wizara yake itatoa ushirikiano kuhakikisha uwekezaji huo unafanyika kwa manufaa ya maendeleo ya sekta ya madini nchini

# Wafanyabiashara, makuli walevi kupewa kibano

Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA

UONGOZI wa Soko Kuu la Singida Mjini umeonya kuwa utamtoza faini mfanyabiashara na mbeba mizigo maarufu kama kulima ya Sh. 10,000 atakayebaini amelewa pombe na kumsimamisha kufanya shughuli zake kwa muda ili kukomesha tabia hiyo.

Hatua hiyo inakuja baada ya kutunga sheria dhidi ya mfanyabiashara wanaojihusisha na ulevi wakati wa biashara wakiwa sokoni hapo.

Adhabu hiyo pia itamhusu mtu yeyote atakayebainika amefika sokoni akiwa amelewa.

Mwenyekiti wa soko hilo, Hassan Mboro alisema hayo jana mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego na Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe na watumishi wengine wakati wakifanya usafi sokoni hapo kiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano yatakayofanyika nchini kesho.

Mboro alisema wameweka sheria hiyo kutokana na baadhi ya wafanyabishara kuendekeza tabia ya kwenda katika soko hilo wakiwa wamelewa chakali na kugeuka kero kwa wateja.

Alisema baadhi ya vijana wanaobeba mizigo maarufu kama makuli kuleta au kutoa katika soko hilo, wamekuwa wakitumia lugha za matusi watakumbana na faini hiyo au kupigwa marufuku kufika sokoni hapo.

"Unakuta kijana amepatana na mfanyabiashara kubeba mzigo wake mfano kwa Sh. 5,000 lakini akishaufikisha anamgeuka anasema walipatana kwa Sh.10,000 na kuanza kutoa lugha za matusi jambo tumeona ili kulikomesha ni kumkamata na kumtoza faini hiyo," alisema Mboro.

Alisema kwa mfanyabiashara ambaye atatozwa faini, atakumbana na adhabu nyingine ya kutoruhusiwa kufika sokoni hapo kwa siku saba au 14 na kurejea na mdhamini wake ili kama akirudia kosa, afukuzwe moja kwa moja.

Akizungumza na wananchi katika soko hilo baada ya kufanya usafi, Dendego alionya kuwa atawachukulia hatua kali mtu au kikundi cha watu wanaotaka kuvuruga amani na utulivu katika mkoa huo.

Aliwasisitiza wakazi wa mkoa huo kuwakataa watu au kikundi kinachotaka kumdhalilisha Rais Samia Suluhu Hassan vingine watakuwa wamedhalilisha Taifa na Watanzania wenzao.

"Tuungane wote katika kupambana na yeyote anayetaka kuleta ujinga ujinga katika Taifa letu tuwabaini ili tuwawajibishe," alisema.

Alisema kwa kuwa yeye ni rafiki wa wote vijana, wazee na wanawake, ofisi yake ipo wazi kwa anayetaka msaada kwani nia yake ni kuona wakazi wa Singida wanaishi maisha mazuri na yenye staha.

Kwa upande wake, Gondwe alimhakikishia mkuu huyo wa mkoa kusimamia maelekezo aliyotoa ya kuhakikisha maeneo ya Manispaa ya Singida yanakuwa safi ili kudhibiti magonjwa ya mlipuko kikiwemo kipindupindu.

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

# MWITO WA KUTOA MAONI KUHUSU MAOMBI YA VIBALI VYA UJENZI NA LESENI KUTOKA EWURA

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni Taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 126 (1) cha sheria ya mafuta kinamtaka mtu yoyote anayetaka kujenga miundombinu ya mafuta kuomba kibali cha ujenzi kutoka EWURA. Aidha, Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

EWURA imepokea maombi ya vibali vya ujenzi kwa ajili ya kujenga miundombinu ya mafuta na leseni ajili ya kujihusisha na biashara/shughuli katika mkondo wa kati na chini wa sekta ya mafuta ya petroli kutoka kwa waombaji walioorodheshwa hapa chini. Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma juu ya maombi haya ya leseni na vibali vya ujenzi.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Kibali Cha Ujenzi/leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Olympic Petroleum (T) Limited, S.L.P 16484, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "AA", Eneo la Ihumwa, Mapinduzi, Dodoma. | Ally Adon (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 2. | Petroafrica (T) Limited - Ndachi Service Station, S.L.P 4878, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 299, Kitalu "AJ", Eneo la Ndachi, Mnadani, Dodoma. | Yassin Warsame (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 3. | Mount Meru Petroleum Limited, S.L.P 7094, Arusha. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "NC", Eneo la Ihumwa, Dodoma. | Atul Mittal (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 4. | Afroil Investment Limited, S.L.P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 233, Kitalu "BE", Eneo la Miyuji, Dodoma | Hilmy Ahmed Mbarak (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 5. | Vel Estates Company Limited, S.L.P 77715, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 94, Kitalu "ZA", Eneo la Mtumba, Dodoma. | Vicent Elifatio Lyimo (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 6. | Mohamed Mansour Huwel T/A Sheli Energy Company Limited, S.L.P 839,Iringa. | Kiwanja Na. 38, Kitalu "C", Eneo la Viwanda, Morogoro. | Mohamed Mansour Huwel (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 7. | Mwalo Opiyo Mboga T/A Igingilanyi Petroleum Limited, S.L.P 1263,Iringa. | Kiwanja Na. 4, Kitalu "C", Eneo la Igingilanyi, Kising'a, Iringa. | Mwalo Opiyo Mboga (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 8. | Hachoki Investments Company Limited, S.L.P 340, Karagwe. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "B", Eneo la Nyakasimbi, Karagwe, Kagera. | Simon Angelo Kafuba (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 9. | Celestine Rweumbiza Kazoba, S.L.P 34144, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 5, Kitalu "D", Eneo la Nyaishozi, Karagwe, Kagera. | Celestine Rweumbiza Kazoba (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 10. | Martin Valentine Orwanda, S.L.P 47, Rorya, Mara. | Kijiji cha Irienyi, Komuge, Rorya, Mara. | Martin Valentine Orwanda (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 11. | Afroil Investment Limited, S.L.P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 5, Kitalu "K", Eneo la Mpemba – Tunduma, Momba, Songwe. | Hilmi Ahamed Mbaraka (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 12. | Sichuan Road and Bridge Corporation Ltd, S.L.P 6016, Dar es Salaam. | Eneo La Jangwani, Wilaya a Ilala, Dar es Salaam. | Zhu Jiankun (Raia Wa China) | Kibali Cha Ujenzi wa Miundombinu ya Kutunzia Condensate |

# TANGAZO

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Kibali Cha Ujenzi/leseni |
|---|---|---|---|---|
| 13. | Pyramid Oil Company S.L.P 2473 Dar es Salaam | Kiwanja Na. 54, 55 & 56, Kitalu "Q", Eneo La Buyuni, Ilala, Dar es Salaam. | Sebastian John Luena (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 14. | ATN Petroleum Co. Ltd, S.L.P 683, Morogoro. | Kiwanja Na. 29632, Eneo La Ubungo Mkuburi, Ubungo, Dar es Salaam. | Abdulatif Taalib Mohamed (Mtazania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 15. | Mainline Carriers Limited, S.L.P 42804, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 91/92, Eneo La Mbagala, Temeke, Dar es Salaam. | Marinus Forune Christian Dom (Raia Wa Zimbabwe) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 16. | Lavechi Mbughi Investment Limited, S.L.P 55068, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P31578, Eneo La Maramba Mawili, Ubungo, Dar es Salaam. | Lazaro Mbughi (Mtazania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 17. | Mustafa Salehe Matala S.L.P 268, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 37, Eneo la Msongola, Ilala, Dar es Salaam. | Mustafa Salehe (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 18. | Xtra Energies Company Limited, S.L.P 13656, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 60, Kitalu "B", Eneo la Chamazi, Temeke, Dar es Salaam. | Bilal Nahdi (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 19. | Idrisa Ally Kiluvia, S.L.P 61071, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 163, Kitalu "C", Eneo la Msangani, Kibaha, Pwani. | Idrisa Ally Kiluvia (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 20. | Bestie Energy, S.L.P 90005, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "Z", Eneo La Chamakweza, Bagamoyo, Pwani. | Yusuph Amani Maimu (Mtazania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 21. | Unique Energy Company Limited, S.L.P 7971, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 8, Kitalu "F", Kibaha, Pwani. | Fatma Salmin Badaar (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 22. | Deo I. Assenga Company Limited, S.L.P 8570, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 12, Kitalu "E", Eneo la Mjimwema, Chalinze, Pwani. | Deogratias Isdori Assenga (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 23. | Petroafrica (T) Limited - Lindi, S.L.P 4878, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "V", Eneo la Matopeni, Lindi. | Yasin Warsame (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 24. | Gapco Tanzania Limited – Mbey Gapco Service Station, S.L.P 9103, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 6A, Kitalu "5" Barabara ya Lupa, Sisimba, Mbeya. | Jean-francois Schoepp (Raia wa Ubeligiji) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 25. | Malongo Isack James Petrol Station, S.L.P 34,Rujewa. | Ubaruku, Mbarali, Mbeya. | Malongo Isack James (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 26. | Oryx Energies Tanzania Limited – Vwawa Service Station, S.L.P 9540, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 57, Kitalu "F", Vwawa, Mbozi, Songwe. | Kalpesh Mehta (Raia wa Uingereza) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 27. | Ngara Oil Tanzania Limited - Rulenge, S.L.P 318, Ngara, Kagera. | Kijiji cha Munjebwe, Mubosoro, Ngara, Kagera. | Ally Suleiman Hilal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 28. | Laulian Burukadi Katarama - Murusagamba, S.L.P 150, Sengerema, Mwanza. | Kijiji cha Murusagamba, Mawe Matatu, Ngara, Kagera. | Laulian Burukadi Katarama (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 29. | Nicodemus Henry Maganga T/A Masumbwe Petrol Station, S.L.P 22, Masumbwe, Mbogwe, Geita. | Kiwanja Na. 18, Kitalu "A", Eneo la Masumbwe, Mbogwe, Geita. | Nicodemus Henry Maganga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 30. | NGS Petroleum Limited - Lwamgasa, S.L.P 20, Bariadi, Simiyu. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "A" Eneo la Lwamgasa, Geita. | Njalu D. Silanga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 31. | Suleiman Hassan Rwaikondo, S.L.P 116, Chato. | Kiwanja Na. 455, Kitalu "A" Eneo la Ibondo – Buseresere, Chato, Geita. | Suleiman Hassan Rwaikondo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 32. | Muriba Oil, S.L.P 336, Tarime. | Kijiji cha Muriba, Tarime, Mara. | Matiko Silasi Maisa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 33. | NGS Petroleum Limited - Lagangabilili, S.L.P. 20, Bariadi, Simiyu. | Kijiji cha Lagangabilili, Itilima, Simiyu. | Njalu D. Silanga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 34. | Oryx Energies Tanzania Limited - Isaka Service Station, S.L.P 9540, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 407 - 412 Kitalu "A", Eneo la Isaka, Kahama, Shinyanga. | Kalpesh Mehta (Raia wa Uingereza) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 35. | Bustemma Universal Traders Limited, S.L.P 32604, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 50, kitalu "JJ", Eneo la Unyankhae, Singida. | Steven Mhele Marwa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 36. | Ester Oil - Mwaya Filling Station, S.L.P 44, Mahenge, Ulanga. | Kiwanja Na. 55 & 57, Kitalu "D", Eneo la Mwaya, Ulanga, Morogoro. | Josephat Steven Madinga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 37. | Camel Oil (T) limited, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 365/366, Eneo la Kurasini, Temeke, Dar es salaam. | Edhah Munif (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 38. | Manjis Gas Supply Company Ltd, S.L.P 41088, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 80-81, Eneo la Vijibweni, Kigamboni, Dar es Salaam. | Rizwan Sajan (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Gesi ya kupikia (LPG) |
| 39. | Jaguar Petroleum Limited, S.L.P 72838, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 331, Eneo la Msasani, Kinondoni, Dar es Salaam. | Tumwesige Evans Lushakuzi (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Gesi ya kupikia (LPG) |
| 40. | UK Eagle Tanzania Pvt Limited, S.L.P 23197, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 369, Eneo la Oysterbay Masaki, Kinondoni, Dar es salaam. | Avinash Santosh Totani (Raia wa India) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 41. | Dalbit Trading, S.L.P 9122, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 1403, Eneo la Msasani, Kinondoni, Dar es Salaam. | Bambino Matawana (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 42. | Toyota Tanzania Limited, S.L.P 9060, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 242, Eneo la Vingunguti, Ilala, Dar es salaam. | Jatin Mahendra Pandya (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 43. | Chemicals and Refined Oil Products (Crop) Limited, S.L.P 21755, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1687, Kitalu 206, Eneo la Keko, Temeke, Dar es salaam | Nassif Bachaalani (Raia wa Lebanon) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi |
| 44. | Royal Soap & Detergent Ind. Ltd S.L.P 22196, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.1, Kitalu "A", Eneo la Mabibo, Ubungo, Dar es Salaam. | Dixita Mohamed Dewji (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi |
| 45. | Saturn Corporation Limited, S.L.P 77007, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2-11, Eneo la Kisarawe II, Kigamboni, Dar es Salaam. | Chirat Kiritkumar Tanna (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta Kwa Matumizi Binafsi |
| 46. | Darpco Energy Limited- Tabata Station, S.L.P 3872, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2077, Eneo la Tabata Liwiti, Ilala, Dar es Salaam. | Thabit Geaorge Mkassi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta. |
| 47. | Africa Energy Ltd, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 547, Kitalu "R", Eneo la Tandika, Temeke, Dar es Salaam. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 48. | Oryx Mbezi Masana Service Station, S.L.P 9540, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 181, Kitalu "C", Mbezi Juu Masana, Kinondoni, Dar es Salaam. | Kalpesh Mehta (Raia wa Uingereza) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 49. | Africa Energy Ltd, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 547, Kitalu "R", Eneo la Tandika, Temeke, Dar es Salaam. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 50. | Africa Energy Ltd, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 44 & 45, Eneo la Mandela Road, Chang'ombe, Temeke, Dar es salaam. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 51. | Lake Oil Limited Mbezi Beach Africana, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2449 & 2450, Eneo La Afrikana, Kinondoni, Dar es Salaam. | Ally Edha Awadh. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 52. | Dubai Energies Company Limited, S.L.P 15018, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P30807, Eneo la Mbezi Mshikamano, Ubungo, Dar es Salaam. | Alfred Arobogst Tarimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 53. | Wael Petrol Station, S.L.P 15333, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 430, Eneo La Amani Gomvu, Kigamboni, Dar es Salaam. | Ally Awadh Abeid (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 54. | Gudal (T) Ltd- Ubungo Kibangu Service Station, S.L.P 216, Nzega. | Kiwanja Na. 29 Kitalu "B", Eneo la Ubungo Kibangu, Ubungo, Dar es Salaam. | Mohamed Mussa Abdillahi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 55. | Backbone Tanzania Company Limited, S.L.P 38675, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 80-84, Kitalu "A", Eneo la Misugusugu, Kibaha, Pwani. | Ming Zhuang (Raia wa China) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 56. | Renatus Hemed Kituranya, S.L.P 40016, Dar es Salaam | Kijiji Cha Dondo, Mkuranga, Pwani. | Renatus Hemed Kituranya (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 57. | Vivo Energy Tanzania Limited, S.L.P 78470, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 83, Kitalu "A", Eneo la Mkomaido, Masasi, Mtwara. | Emmanuel Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote aliyetajwa hapo juu kwamba asipewe leseni au Kibali cha ujenzi, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**

**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005**
**Namba ya Bure 0800110030**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**DICKSON WILLIAM MSUYA** anatangaza kupotelewa kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 149898** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 26/07/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/70179/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU ELIAS AMRI TEIKWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T202 DLK** aina ya **TOYOTA LANDCRUISER,** Rangi Nyeupe.Yenye Engine No.**1HZ0669150** na Chasis No.**JTEEB71J807012254.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **PHQ/KIG/KIB/727/2024.**

## KUPOTEA KADI KWA KADI YA GARI

**ENGLIBERT THOMAS KAYOMBO,** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Audi Q5 yenye no za usajili **T742 DYN, ENGINE NO CDN06081H.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/4971/2024**

## TAARIFA YA KUFUNGWA

**INATOLEWA TAARIFA KUWA** katika mkutano wa ziada wa **GRAVITA VENTURES LIMITED** uliofanyika siku ya 16th ya April 2024, azimio maalum lilipitishwa kwa pamoja na wamiliki/wanahisa wa kampuni la kufunga kampuni kwani haijafanya shughuli zake.

Ikiwa mtu ana madai yoyote au maslahi dhidi ya kampuni, wanashauriwa kuwasiliana na kampuni kwenye anwani iliyo chini ndani ya siku 7 za taarifa hii.

**Karimjee Attorneys**
**P.O. Box 76421**
**Dar es Salaam**

## KUPOTEA KWA HATI ZA KIWANJA NA HOTEL.

**FIDELIS GREGORY FERNANDES** anatangaza kupotea kwa hati ya kiwanja chenye **PLOT NO. 152/2 BLOCK KB 11** na hati ya Hotel yenye **PLOT NO. 1 BLOCK Z.** Kwa yeyote atakaezionа atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **TAN/TAN/RB/420117/2019**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 8495 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**DOROTH PETER MWAKYUSA..............DECEASED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATIX BY**
**ABDUL RAMADHANI DUMWALA..........PETITIONER**
**CITATION**

**(Made under rule 75 of the probate and Administration of Estate rules, CAP 352 R.E 2019)**

ALL person claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 20th day of May 2024.
Dated at Morogoro this 20th day of 04 2024.

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MKURANGA**

**MAOMBI NAMBA 06 YA 2024**

**HENRY SHUZA BITEGEKO....................................MDAI**

**DHIDI YA**

**SAID ABDULAHMAN MTUPA.....................MDAIWA 1**
**MOHAMED NASSORO.................................MDAIWA 2**
**BENJAMIN LUSINDE.................................MDAIWA 3**
**FRANCIS OSCA........................................MDAIWA 4**
**SADOCK GADIEL.......................................MDAIWA 5**
**ADEGUNDA MKONGWA..............................MDAIWA 6**

**KUITWA SHAURINI**

1. **SAID ABDULAHMAN MTUPA**
2. **MOHAMED NASSORO**
3. **BENJAMIN LUSINDE**
4. **FRANCIS OSCA**
5. **ADEGUNDA MKONGWA**

**Popote Mlipo,**
**HENRY SHUZA BETEGEKO**
Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Mkuranga . Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 21.05.2024 mbele ya R. Mwakibuja Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo basi mnatakiwa kuleta utetezi wenu ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba MKURANGA. Endapo hamtatekeleza haya shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 27.03.2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) - MKURANGA

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 61 LA 2024**
**(1) ANICET ASSEY**
**(2) GEORGE NGOMBALEMWIRU................WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**(1) GENIE INTERNATIONAL CO. LTD**
**(2) OMARY KIAKURWA......................MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**(1) GENIE INTERNATIONAL CO. LTD**
**(2) OMARY KIAKURWA..................POPOTE ULIPO/MLIPO**
(1) ANICET ASSEY
(2) GEORGE NGOMBALEMWIRU wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 19/6/2024 saa TATU Asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 22 Mwezi wa 04/2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

TANGAZO

KCBL
Together, Transforming Lives

# KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED (KCBL)

## PUBLICATION OF AUDITED FINANCIAL STATEMENTS

**Issued pursuant to regulations 7 and 8 of the Banking and Financial Instituions (Disclosures) Regulation, 2014**

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31ST DECEMBER 2023
(Amounts in '000' shillings)

| | | Current Year 31st Dec 2023 | Previous Year 31st Dec 2022 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **ASSETS** | | |
| 1 | Cash | 153,897 | 122,302 |
| 2 | Balances with Bank of Tanzania | 593,293 | 480,936 |
| 3 | Balances with other banks and financial institutions | 1,477,957 | 662,153 |
| 4 | Investments in Government securities | 4,708,764 | - |
| 5 | Cheques and items for clearing | - | - |
| 6 | Inter branch float iterms | - | - |
| 7 | Bills negotiated | - | - |
| 8 | Customers' liabilities for acceptances | - | - |
| 9 | Interbank Loans Receivables | - | - |
| 10 | Investments in other securities | 7,304,528 | 2,095,949 |
| 11 | Loans, advances and overdrafts (net of allowances for probable losses) | 8,762,372 | 7,493,647 |
| 12 | Other assets | 161,386 | 337,139 |
| 13 | Equity Investments | - | - |
| 14 | Underwriting accounts | - | - |
| 15 | Property, Plant and Equipment | 2,659,041 | 366,706 |
| **16** | **TOTAL ASSETS** | **25,821,237** | **11,558,832** |
| **B.** | **LIABILITIES** | | |
| 17 | Deposits from other banks and financial institutions | - | - |
| 18 | Customer deposits | 9,327,708 | 5,923,744 |
| 19 | Cash letters of credit | - | - |
| 20 | Special deposits | - | - |
| 21 | Payment orders/transfers payable | - | - |
| 22 | Bankers' cheques and drafts issued | - | - |
| 23 | Accrued taxes and expenses payable | - | - |
| 24 | Acceptances outstanding | - | - |
| 25 | Interbranch float items | - | - |
| 26 | Unearned income and other deferred charges | - | - |
| 27 | Other liabilities | 185,948 | 1,233,998 |
| 28 | Borrowings | - | - |
| 29 | **TOTAL LIABILITIES** | **9,513,657** | **7,157,742** |
| 30 | **NET ASSETS/(LIABILITIES)(16 minus 29)** | **16,307,580** | **4,401,090** |
| **C.** | **SHAREHOLDERS' FUNDS** | | |
| 31 | Paid up share capital | 24,987,034 | 15,305,153 |
| 32 | Capital reserves | 88,892 | (65,457) |
| 33 | Retained earnings | (10,992,955) | (11,165,866) |
| 34 | Profit (Loss) account | 423,349 | 327,260 |
| 35 | Other capital accounts | 1,801,261 | - |
| 36 | Minority Interest | - | - |
| 37 | **TOTAL SHAREHOLDERS' FUNDS** | **16,307,580** | **4,401,090** |
| 38 | Contingent liabilities | - | - |
| 39 | Non performing loans & advances | 301,674 | 166,808 |
| 40 | Allowances for probable losses | 83,916 | 72,945 |
| 41 | Other non performing assets | | |
| **D.** | **SELECTED FINANCIAL CONDITION INDICATORS** | | |
| (i) | Shareholders Funds to total assets | 63.16% | 38.08% |
| (ii) | Non performing loans to total gross loans | 3.41% | 2.20% |
| (iii) | Gross loans and advances to total deposits | 94.85% | 127.73% |
| (iv) | Loans and advances to total assets | 33.93% | 64.83% |
| (v) | Earning assets to Total Assets | 34.15% | 76.07% |
| (vi) | Deposits Growth | 57.46% | 3.97% |
| (vii) | Assets growth | 123.39% | 44.01% |

### STATEMENT OF COMPREHENSIVE INCOME FOR THE YEAR ENDED 31ST DECEMBER 2023
(Amounts in '000' shillings)

| | | Current Year 31st Dec 2023 | Previous Year 31st Dec 2022 |
|---|---|---|---|
| 1 | Interest Income | 1,629,543 | 937,564 |
| 2 | Interest Expense | 139,612 | 47,025 |
| 3 | Net Interest Income ( 1 minus 2) | **1,489,931** | **890,539** |
| 4 | Bad Debts Written -Off | - | - |
| 5 | Impairment Losses on :Loans and Advances | 10,971 | (1,787) |
| **6** | **Non Interest Income:** | **325,643** | **694,658** |
| | 6.1 Foreign Currency Dealings and Translation Gains/ (Loss) | - | - |
| | 6.2 Fees and Commissions | 308,087 | 309,531 |
| | 6.3 Dividend Income | | |
| | 6.4 Other Operating Income | 17,556 | 385,127 |
| **7** | **Non Interest Expenses:** | **1,345,240** | **1,217,369** |
| | 7.1 Salaries and Benefits | 528,764 | 503,285 |
| | 7.2 Fees and Commission | - | - |
| | 7.3 Other Operating Expenses | 816,476 | 714,084 |
| **8** | **Operating Income/ (Loss)** | **459,363** | **369,615** |
| **9** | **Income Tax Provision** | **36,014** | **42,355** |
| **10** | **Net Income / (Loss) After Income Tax** | **423,349** | **327,260** |
| **11** | **Other Comprehensive Income (itemize)** | **1,787,070** | |
| **12** | **Total Comprehensive Income/(loss) for the year** | **2,210,419** | **327,260** |
| 13 | Number of Employees | 24 | 23 |
| 14 | Basic Earnings Per Share | 0 | 0 |
| 15 | Number of Branches | 1 | 1 |
| **SELECTED PERFORMANCE INDICATORS** | | | |
| (i) | Return on Average Total Assets | 1.64% | 2.83% |
| (ii) | Return on Average Shareholders' Fund | 2.60% | 7.44% |
| (iii) | Non Interest Expense to Gross Income | 69.36% | 74.47% |
| (iv) | Net Interest Income to Average Earning Assets | 16.84% | 125.46% |

### STATEMENT OF CASH FLOWS FOR THE YEAR ENDED 31ST DECEMBER 2023
(Amounts in '000' shillings)

| | | Current year 31st Dec 2023 | Previous year 31st Dec 2022 |
|---|---|---|---|
| I: | **Cash flow from operating activities:** | | |
| | Net income (Loss) | 576,152 | 369,614 |
| | **Adjustments for:** | | |
| | - Impairment/Amortization | 63,849 | 38,752 |
| | - Prior Year Adjustment | | - |
| | - Depreciation | 85,170 | 66,245 |
| | - Net change in Loans and Advances | (1,204,186) | (2,855,662) |
| | - Gain/loss on Sale of Assets | - | - |
| | - Net change in Deposits | 3,403,964 | 496,480 |
| | - Net change in Short Term Negotiable Securities | - | - |
| | - Net change in Other Liabilities | (1,051,635) | 956,093 |
| | - Net change in Other Assets | (77,233) | (255,245) |
| | - Tax Paid | (30,000) | (93,119) |
| | - Others (specify) | | |
| | - Due to other banks | (3,608,129) | (89,406) |
| | ***Net cash provided (used) by operating activities*** | **(1,842,048)** | **(1,366,248)** |
| | | | |
| II: | **Cash flow from investing activities:** | | |
| | Dividend Received | - | - |
| | Purcharse of Fixed Assets | (593,583) | (8,143) |
| | T Bills | (200,375) | - |
| | T Bonds | (6,008,388) | - |
| | Investment | (31,222) | - |
| | Others (Adjustment on Property Plant and Equipment) | (46,509) | (15,414) |
| | ***Net cash provided (used) by investing activities*** | **(6,880,077)** | **(23,557)** |
| | | | |
| III: | **Cash flow from financing activities:** | | |
| | Repayment of Long-term Debt | - | - |
| | Preference share | 7,000,000 | - |
| | Proceeds from Issuance of Share Capital | 2,681,880 | 1,326,163 |
| | Change in Reserve | | - |
| | Net Change in Other Borrowings | - | - |
| | Others (Adjustment in retained earnings) | | - |
| | ***Net Cash Provided (used) by Financing Activities*** | **9,681,880** | **1,326,163** |
| IV: | **Cash and Cash Equivalents:** | | |
| | **Net Increase/ (Decrease) in Cash and Cash Equivalents** | **959,755** | **(63,642)** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the Beginning of the Quarter/Year** | **1,265,392** | **1,329,034** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the end of the Quarter/Year** | **2,225,147** | **1,265,392** |

Godfrey J. Ng'urah
**GENERAL MANAGER** — 4/24/24

Kinyaki O. Kinyaki
**HEAD OF FINANCE AND ADMINISTRATION** — 4/24/24

Apolinary S. Kityamwi
**HEAD OF INTERNAL AUDIT** — 4/24/24

The above extracts are from the financial statements of the Bank for the year ended 31st December,2022 which have been prepared in accordance with International Financial Reporting Standards (IFRS).The financial statements were audited by INNOVEX AUDITORS and received a unqualified report.The financial statements were approved by the Board of Directors on 24th April, 2024 and signed on their behalf by:

| Name | Signature | Date |
|---|---|---|
| 1. Prof. GERVAS M. MACHIMU, CHAIRMAN, BOARD OF DIRECTORS | | 4/24/24 |
| 2. CPA. MWAMINI J. MUSSA, DIRECTOR | | 4/24/24 |

### CONDENSED STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY AS AT 31/12/2023
(Amounts in '000' shillings)

| Current Year | Share Capital | Share Premium | Retained Earnings | Regulatory Reserve | Others | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Balance as at 1st January, 2023** | **15,305,153** | **-** | **(10,969,520)** | **65,457** | **-** | **4,401,090** |
| Profit for the year | | - | 423,349 | - | - | **423,349** |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | **0** |
| Transactions with owners | 9,681,880 | - | - | - | - | **9,681,880** |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | **0** |
| Regulatory Reserve | - | - | (23,435) | 23,435 | - | **0** |
| General Provision Reserve | - | - | | | | **0** |
| Others(Adjustment) | - | - | - | - | | **0** |
| **Balance as at 31st December, 2023** | **24,987,033** | **-** | **(10,569,606)** | **88,892** | **-** | **14,506,319** |
| | | | | | | |
| **Balance as at 1st January, 2022** | **13,978,990** | **-** | **(11,257,904)** | **26,581** | **-** | **2,747,669** |
| Profit for the year | | - | 327,260 | - | - | 327,260 |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | 1,326,163 | - | - | - | - | 1,326,163 |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | 92,038 | (92,038) | - | - |
| General Provision Reserve | - | - | - | - | | - |
| **Balance as at 31st December, 2022** | 15,305,153 | - | (10,838,606) | (65,457) | - | 4,401,090 |
| **Prior Year Adjustment** | - | - | (130,914) | 130,914 | | - |
| **Restated Balance as at 31st December, 2022** | **15,305,153** | **-** | **(10,969,520)** | **65,457** | **-** | **4,401,090** |




Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Absa Tanzania, Aron Luhanga (wa pili kushoto ) akiwa na maofisa wengine mbalimbali wakionyesha fulana maalum zitakazovaliwa na washiriki wa Absa Dar City Marathon itakayofanyika Mei 5, mwaka huu jijini, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ABSA YAENDELEZA UDHAMINI WA DAR CITY MARATHON 2024

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Absa Tanzania imetangaza rasmi kuendelea kudhamini mbio za Absa Dar City Marathon ikiwa ni mwaka wa nne mfululizo kwa lengo la kuifanya jamii kuwa na taifa lenye watu wenye afya njema, imeelezwa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mbio za Absa Dar City Marathon 2024, Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Aron Luhanga, alisema afya njema ni mtaji namba moja katika maendeleo ya Taifa la Tanzania na wanaokimbia wanajenga afya zao.

**Luhanga alisema lengo lingine kuu la Absa Dar City Marathon ni kukusanya fedha kwa ajili ya kuelekeza katika shughuli za kijamii kwa kununua vifaa vitakavyosaidia wodi ya wanawake kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja iliyoko Dar es Salaam.**

"Pamoja na hayo kama kauli mbiu ya mbio hizi isemayo 'Kata Mtaa, Ujue Jiji' sisi kama benki ya Absa, tukiwa na matawi ya kibenki hapa jijini, tunajisikia fahari kusapoti mbio hizi zenye lengo lingine la kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika jiji letu.

Kauli yetu ya Absa inasema 'Story Yako ina Thamani', hivyo tunaamini ukienda kukimbia unaandika Story Yako, ukienda kusaidia jamii, unaandika Story Yako, nasi kama Absa, Story Yako ina thamani sana kwetu," alisema Luhanga.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Klabu ya The Runners, Godfrey Mwangungulu, alisema mbio za mwaka huu zinazofanyika chini ya udhamini mkuu wa Absa Tanzania na zitashirikisha mbio za kilomita 21, kilomita 10 na kilomita tano.

"Absa Dar City Marathon ya mwaka huu inayotarajiwa kufanyika Mei 5, ikianzia kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, ni zaidi ya mbio, ni zaidi ya sherehe, ni kilele cha sherehe za mbio zote zinazoendelea kufanyika hapa nchini.

Tumefanya mbio hizi kwa miaka mitatu mfululizo, mwaka huu tunataka kuzifanya kwa mafanikio zaidi, tunatarajia zaidi ya wanariadha 3,000 kushiriki, tunawashukuru sana wadhamini wetu wakuu, benki ya Absa pamoja na wadhamini wengine," Mwangungulu alisema.

Aliwataja wadhamini wengine ni pamoja na Kampuni ya Alliance Life Assurance, Hill Water, Kilimanjaro Milk na Garda Security.

# Nage wa Zanzibar waahidi makubwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WACHEZAJI wa Timu ya Taifa ya Nage ya Zanzibar ' Zanzibar Blue Queens' wametakiwa kudumisha nidhamu na kwenda kupambana ili kufanya vizuri katika mashindano ya Kombe la Muungano yatakayofanyika kesho jijini, Dar es Salaam.

Kamishna wa Idara ya Michezo Zanzibar, Ameir Mohamed, alisema hayo katika hafla ya kukabidhi Bendera ya Taifa kwa timu hiyo inayoelekea Tanzania Bara kushiriki mashindano ya Kombe la Muungano.

Mohamed alisema Siri ya ushindi katika mchezo wowote duninai inatokana na umoja, heshima na nidhamu kwa viongozi pamoja na kuwaheshimu wachezaji wenzao.

Alisema ni aibu kwa timu ambayo imebeba jina la nchi kushindwa kutunza nidhamu jambo ambalo huenda litasababisha kupata matokeo mabaya.

"Tunatakiwa kuhakikisha tunatimiza nidhamu katika mashindano yote ambayo tunashiriki, siri ya ushindi ni nidhamu na heshima, hivyo tujitahidi katika kulizingatia hili, tunawaangalia nyinyi na tunataka ushindi wenye heshima," alisema Mohamed.

Alilipongeza Shirikisho la Nage Zanzibar (SHENAZA), kwa mara ya kwanza kuteua Timu ya Taifa ya na hiyo inaonyesha mchezo huo umepiga hatua kubwa.

Pia aliwataka waendelee kuwa wabunifu katika kuboresha mchezo huo ambao ni wa asili na unabeba utamaduni wa Zanzibar.

"Mchezo huu kwa sasa umekuwa sana, kwa kifupi tunatakiwa kujivunia kwa sababu ni moja ya alama za utamaduni wa Mzanzibari," Mohammed alisema.

Naye Makamu wa Rais SHANEZA, Fatma Abdallah, alisema kikubwa wanachoahidi ni kurejea nyumbani na ushindi wa 'kishindo' kwa sababu ya maandalizi mazuri waliyofanya.

"Tunaahidi ushindi mkubwa, tumekuwa tukifanya vizuri katika mashindano haya ambayo awali tulishiriki kwa ngazi ya klabu tu, lakini mwaka huu tunapeleka ngazi ya taifa, tunataka kuweka historia," alisema kiongozi huyo.

# ZFF Cup mambo yameiva

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU nane zinazotarajiwa kuchuana katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la ZFF (FA CUP Zanzibar), zimepatikana.

Timu hizo ni KMKM SC, KVZ FC, Mafunzo SC, JKU SC, Zimamoto SC, Uhamiaji FC, Mlandege FC kutoka katika Ligi Kuu Zanzibar na moja inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, Taifa Jang'ombe FC.

Katibu wa Kamati ya Mashindano wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Bakari 'Cheupe' alisema baada ya kukamilika hatua hiyo ya 16 bora, sasa wanajipanga na hatua inayofuata.



Cheupe (pichani) alisema hatua hiyo iliyomalizika ilichezwa kwa mafanikio makubwa kama walivyopanga kwa timu zote kufuata kanuni za mashindano.

Hata hivyo Cheupe alisema licha ya bingwa wa mashindano hayo kupata zawadi ya Sh. milioni 30 zinazotolewa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), bado wanaendelea kusaka wadhamini ili kupata fedha za kusaidia mechi za hatua ya robo fainali, nusu fainali na hatua ya michezo miwili ya fainali.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### ARSENAL, CITY VITANI

ARSENAL na Manchester City inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Newcastle United na Timu ya Taifa Brazil, Bruno Guimaraes, mwenye umri wa miaka 26. ***(Telegraph)***

#### SILVA AITAKA BARCELONA

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Bernardo Silva, ameamua kuondoka Manchester City na nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, ambaye ana kipengee cha kumuachiliwa cha pauni milioni 50 ameonyesha nia ya kuhamia Barcelona. ***(Sport)***

#### LUKEBA ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inamwania mlinzi wa kati wa RB Leipzig na Ufaransa, Castello Lukeba, mwenye umri wa miaka 21, ambaye ana kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 60 katika mkataba wake na klabu hiyo ya Bundesliga. ***(FootMercato)***

#### TEN HAG ATAKA STRAIKA

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag anataka klabu hiyo kumleta mshambuliaji mwingine katika majira ya joto ili kuimarisha safu yake ya ushambuliaji. ***(Goal)***

#### THIAGO KUONDOKA CHELSEA

MLINZI wa Chelsea, Thiago Silva mwenye umri wa miaka 39 amefikia makubaliano ya mdomo na Fluminense, huku Mbrazil huyo akimaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu.***(Goal)***

#### VAN PERSIE KAZINI

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Arsenal na Manchester United, Robin van Persie, anakaribia kuchukua wadhifa wake wa kwanza wa ukocha, baada ya kufanya mazungumzo na klabu inayoshiriki Ligi Kuu Uholanzi, Heerenveen. ***(Algemeen Dagblad)***

#### VAZQUEZ, MADRID SAFI

REAL Madrid inapanga kumwongezea mkataba mlinzi wa Hispania, Lucas Vazquez, mwenye umri wa miaka 32, ambaye mkataba wake wa sasa unakamilika Juni, mwaka huu. ***(AS)***

#### YAMAL ATAKIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inamsaka kinda wa Barcelona mwenye umri wa miaka 16, Lamine Yamal. ***(Le Parisien)***

#### BASTONI KUTUA UNITED

KLABU ya Manchester United inavutiwa na mlinzi wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Italia, Alessandro Bastoni, mwwenye umri wa miaka 25, na wako tayari kutoa takribani pauni milioni 52. ***(Fichajes)***

#### GIL KUONDOKA SPURS

KLABU ya Uholanzi ya Feyenoord inavutiwa na winga wa Tottenham Hotspur mwenye umri wa miaka 23, Bryan Gil, ambaye anatarajiwa kuondoka Spurs msimu wa joto. ***(Standard)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POCHETTINO: WACHEZAJI CHELSEA WALIKATA TAMAA

### Ni baada ya kupokea kipigo 'kizito zaidi' katika dabi ya...

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino alikiri Chelsea "ilikata tamaa" katika kipigo cha mabao 5-0 kutoka kwa Arsenal, lakini aliwatetea wachezaji wake.

**Bao la dakika ya nne la Leandro Trossard lilifungua ukurasa wa magoli kabla ya mabao manne ndani ya dakika 18 za kipindi cha pili, mawili kutoka kwa Ben White na Kai Havertz na kuifanya Chelsea kupata kipigo kizito zaidi katika mchezo wa dabi ya London kwa mara ya kwanza tangu Machi 1986.**

"Tulizungumza wakati wa mapumziko kuhusu jinsi haiwezekani kuanza mchezo kama tulivyofanya," alisema Pochettino.

"Lakini tulianza kipindi cha pili kwa njia mbaya tena. Tuliruhusu mabao mawili na kwa wakati huu, timu ikakata tamaa. Hatukuwa mchezoni.

"Nilicheza mpira wa miguu na nilikuwa katika hali kama hizo na wachezaji wakubwa, wachezaji wenye uzoefu. Nilicheza na Diego Maradona, nilicheza na Ronaldinho, nilicheza na Gabriel Batistuta.

"Katika sehemu fulani ya msimu, aina hizi za vitu inaweza kutokea na ukasema 'ndiyo, hawa watu waliokuwa juu na tulikata tamaa.

"Wakati mwingine kwa sababu ya mpinzani, kwa sababu ya nguvu zetu, kwa sababu hakuna kitu kwa ajili yako katika hali hii na huwezi kupata chochote chanya wakati wa mchezo na aina hii ya kitu hutokea. Itatokea kwa hakika na timu tofauti."

Wakati Arsenal wakisonga mbele kwa pointi nne dhidi ya Manchester City wakiwa kileleni baada ya kucheza michezo miwili zaidi, huku Liverpool wakiwa katika nafasi ya pili, Chelsea wanakabiliwa na hatari ya kukosa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

"Tuna uwezo wa kufanya vizuri na siku tatu baadaye, tunaonyesha viwango vya juu," aliongeza Pochettino.

"Viwango vyetu haviendelezwi kwa siku mbaya, tukiwa na siku mbaya tunakuwa wabaya sana, tunapokuwa wazuri tuna uwezo wa kila kitu, ni jambo lingine tunapaswa kufahamu kuongezeka kwa siku zijazo."

# RODRYGO AKANUSHA KUTAKIWA ENGLAND




**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Rodrygo amejitenga na uvumi anaweza kuondoka katika klabu hiyo huku kukiwa na tetesi za kutakiwa Ligi Kuu England (EPL).

Licha ya kurekodi msimu wake bora wa ufungaji kwenye LaLiga (10) hadi sasa na kuchukua jukumu kubwa katika mafanikio ya Madrid miaka ya hivi karibuni, Rodrygo amekuwa akihusishwa na kuondoka kwa sababu ya ujio wa Kylian Mbappe.

Ripoti nchini Hispania mwezi uliopita zilidai Manchester United, Liverpool, Arsenal na Manchester City zote zinamtaka Rodrygo, huku Paris Saint-Germain pia ikihusishwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.

Lakini Rodrygo mwenyewe hana mpango wa kuondoka pale Bernabeu.

"Naipenda klabu hii sana," aliambia beIN SPORTS.

"Natumaini maisha yangu ya baadaye yatakuwa hapa kila wakati. Carlo Ancelotti ni kama baba kwangu."

Rodrygo alikuwa na umri wa miaka 17 tu wakati Madrid ilipokubali kumsajili kutoka Santos mwaka 2018.

Inaeleweka Rodrygo alikuwa mchezaji asiye na uwezo alipowasili mara ya kwanza lakini alifurahia jambo la kampeni ya 2021/22 alipocheza mara 49 katika mashindano yote na kufunga mabao muhimu katika mechi za mtoano za Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Chelsea na Manchester City.

Rodrygo alikabidhiwa jezi namba 11 ya Madrid msimu uliopita wa joto baada ya kuachwa na Marco Asensio.

# Giroud atimkia Marekani

**LOS ANGELES,** Marekani

MSHAMBULIAJI wa AC Milan, Olivier Giroud, amesaini mkataba wa kujiunga na Los Angels FC inayoshiriki Ligi Kuu ya Soka Marekani, kuanzia katikati ya Julai hadi Desemba, 2025, kwa mujibu wa ESPN.

Baada ya wiki kadhaa za mazungumzo na licha ya ofa nyingine kutoka Saudi Arabia na Ulaya, nyota huyo wa zamani wa Arsenal na Chelsea aliamua kukubali ofa ya LAFC ambapo atalipwa euro milioni tatu kwa msimu.

Alikutana na John Thorrington, Rais Mwenza wa LAFC, huko Milan kutia saini mkataba wake, huku Giroud akitarajia kuwa sura mpya katika maisha yake huko Los Angeles.

Giroud mwenye umri wa miaka 37, ataungana na rafiki yake na mchezaji mwenzake aliyeshinda Kombe la Dunia la 2018, Hugo Lloris, ambaye alisajiliwa na LAFC katika dirisha dogo.




Amefunga mabao 13 na kutoa asisti nane katika michezo 30 akiwa na Milan msimu huu na bado yuko kwenye kikosi cha Ufaransa cha Didier Deschamps.

Giroud ndiye mfungaji bora wa Ufaransa (amefunga mabao 57 katika mechi 131).

Atajiunga na LAFC baada ya kushiriki Euro 2024 nchini Ujerumani, ambapo Les Bleus wanapewa nafasi kubwa ya kutwaa taji hilo.

Habari za Giroud kusaini mkataba wake na LAFC ziliripotiwa kwanza na Fabrizio Romano.

MLS itakuwa ligi ya sita tofauti kwa Giroud katika maisha yake ya soka baada ya kuanza Ligi Daraja la Tatu, Ligue 2 na Ligue 1 nchini Ufaransa akiwa na Grenoble, Istres, Tours na Montpellier, ambapo alishinda taji la Ufaransa mwaka 2012.

Kisha akahamia Ligi Kuu England, kwanza akiwa na Arsenal, ambako alishinda mataji matatu ya FA, halafu Chelsea, ambako alinyanyua Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi ya Europa na Kombe la FA.

Alijiunga na Milan mwaka 2021, akishinda taji la Serie A katika msimu wake wa kwanza.

Giroud amekuwa mfungaji wa kutegemewa katika ngazi ya klabu, akifunga mara 276 katika maisha yake ambayo yamechukua takriban mechi 700 za ligi na mataji.

Alikuwa sehemu ya timu ya Ufaransa iliyoshinda Kombe la Dunia mwaka 2018, akicheza katika mechi zote saba.

Giroud pia aliiwakilisha Ufaransa katika michuano mingine miwili ya Kombe la Dunia na michuano mitatu ya Ulaya.

## Liverpool wamgeukia Slot

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imemtambua Kocha wa Feyenoord, Arne Slot, kama mwalimu anayeongoza mbio za kurithi mikoba ya Jurgen Klopp, baada ya kupunguza nia yao ya kumchukua Ruben Amorim wa Sporting CP, kwa mujibu wa ESPN.

Huku mlengwa Mkuu akiwa, Xabi Alonso, alijiondoa katika kinyang'anyiro cha kurejea katika klabu aliyoiwakilisha kama mchezaji kwa kuchagua kusalia na mabingwa wapya wa Bundesliga, Bayer Leverkusen, Slot ameibuka mbele ya Amorim na Roberto De Zerbi wa Brighton.

Hata hivyo, vyanzo vimesema Liverpool wanatarajia vita na Barcelona na Bayern Munich katika kumwania Slot, hivyo wanapanga kuendelea kutathmini wagombea wengine.

Klopp, ambaye ameshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu England akiwa na Liverpool tangu kuchukua nafasi ya Brendan Rodgers hapo Anfield mnamo Oktoba mwaka, 2015, alitangaza Januari atajiuzulu kutoka nafasi yake mwishoni mwa msimu huu.



Kufuatia tangazo la mshangao la Klopp, mwenye umri wa miaka 56 aliwafahamisha wamiliki wa Liverpool, Fenway Sports Group (FSG) juu ya uamuzi wake Novemba, mwaka jana.

Mkurugenzi Mtendaji wa Liverpool, Billy Hogan, alisema kuwa klabu hiyo itachukua mbinu "iliyoongozwa na data" kutafuta kocha mpya.

Mkurugenzi wa zamani wa michezo, Michael Edwards, alirejea Anfield mwezi uliopita kama mkuu wa shughuli za soka akiwa na jukumu la kumtambua na kuajiri mrithi wa Klopp, na vyanzo vimeiambia ESPN Slot, ambaye aliiongoza Feyenoord kutwaa ubingwa wa Uholanzi msimu uliopita, amekuwa mshindani mkubwa wa kuchukua hiyo.

Slot mwenye umri wa miaka 45, alikataa ofa za Ligi Kuu England kutoka kwa Chelsea na Tottenham Hotspur msimu uliopita ili kusalia Feyenoord.

HABARI MICHEZO

## Mo kufanya 'kufuru' usajili

INATOKA UKURASA 24

anatakiwa na FAR Rabat ya Morocco," chanzo hicho kiliongeza.

Alisema pia nafasi ambazo wanataka kuziboresha ni mabeki wawili wa kati, kiungo, winga na washambuliaji.

"Bosi amedhamiria kusimamia kwa karibu mchakato wa usajili, anataka kuona wachezaji wenye ubora na kiwango kizuri wanatua kuja kusaidia timu, tufanye vizuri katika mashindano yote ya msimu ujao. Kushindwa kufikia malengo ya kucheza nusu fainali na kupoteza matumaini ya kutwaa ubingwa wa ligi, kuondolewa kwenye kombe la FA ni moja ya sababu ya bosi (Mo) kufanya kikao na viongozi wa klabu na washauri wake ili kujipanga upya," aliongeza mtoa habari huyo.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alikiri ni kweli kikosi chao kinahitaji maboresho lakini kwa sasa nguvu na akili zimeelekezwa katika kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo ya Ligi Kuu iliyobakia.

Ahmed alisema wanahitaji kupambana ili kumaliza msimu katika nafasi ya pili na watafikia malengo hayo kwa kufanya vizuri kwenye mechi zote zilizosalia.

"Ni kweli maboresho yatafanyika tena maboresho makubwa, tutajenga timu imara, kwa sasa tunatakiwa tujikite zaidi katika michezo iliyosalia ya ligi kwa kudumisha umoja wetu, kuwapa ushirikiano mzuri viongozi na wachezaji," alisema Ahmed.

## Yanga SC yapunguzwa

INATOKA UKURASA 24

kusababisha kizaazaa cha piga nikupige, lakini alifanikiwa tena kuudhibiti mikononi.

Timu zote zilifanya mabadiliko ambayo yalionekana kutoathiri mwenendo wa mchezo, huku kila timu ikikosa mabao.

Sixtus Sabilo, ataikumbuka nafasi aliyopata dakika ya 75, alipopenyezewa pasi maridadi kutoka kwa Hassan Kapalata, akiwa anaangaliana na Diarra, alipaisha mpira juu, akiwa ndani ya eneo la boksi.

Aziz Ki aliunganisha vibaya mpira wa krosi kutoka kwa Kouassi dakika ya 79, ukaenda nje akiwa katika nafasi nzuri ya kuukwamisha mpira wavuni.

Yanga itajutia nafasi iliyokosa katika dakika tano zilizoongezwa, ambapo krosi iliyopigwa kutoka wingi ya kushoto ilimkuta, Joseph Guede, aliyeunganisha, lakini mpira ukaenda kugonga mwamba wa juu na kudunda chini katikati ya mstari na mwamba wa pembeni ukarejea uwanjani, kabla ya kipa Jacob, hajaudaka.

# SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS DABI YA KISASI

**Na Saada Akida**

"WANAENDA kulipa kisasi cha kaka zetu". Hiyo ni kauli ya Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', kuelekea mechi ya Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania dhidi ya watani zao wa jadi, Yanga Princess itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

**Vinara Simba Queens wenye pointi 31 watashuka uwanjani leo wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-1 walioupata katika mechi ya kwanza wakati Yanga Princess wako nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo wakiwa na alama 21.**

Licha ya mchezo huo kuwa dabi, Simba Queens wamejipanga kuhakikisha wanalipa kisasi cha 'kaka zao' Simba ambao walikubali kipigo cha pili msimu huu dhidi ya Yanga.

Akizungumza jijini jana, Mgosi alisema wamejiandaa vizuri kusaka pointi tatu muhimu lakini kubwa kwao no kulipa kisasi walichofanyiwa kaka zao, Simba.

Mgosi alisema wamefanya maboresho ba kusahihisha mapungufu waliyoyabaini katika kikosi chao na wataingia tofauti na namna walivyocheza mechi yao ya mwisho dhidi ya Baobab Queens.

"Yanga Princess wapo vizuri lakini hata Simba Queens tuko vizuri kupambania malengo yetu, tunahitaji kutwaa ubingwa, hatuwezi kufikia hapo hadi kuvuna pointi tatu katika kila mechi, mashabiki wanatakiwa kujitokeza kwa wingi kutuunga mkono.

Kufuatia kile ambacho wamekipata kwa kaka zetu wikiendi iliyopita na mashabiki wetu kupata maumivu tunawahakikisha tunaenda kulipa kisasi cha kaka zetu, hatuna kazi mbovu, tunaenda kucheza soka safi lakini kuhakikisha tunawapa furaha mashabiki wetu," alisema Mgosi

Nahodha wa Simba Queens, Violeth Nicholaus, alisema wamejipanga vizuri sio kwa mchezo wa leo pekee, ila wanahitaji kutafuta pointi tatu mbele ya mpinzani yoyote wanayekutana naye katika ligi hii.

"Msimu huu tunahitaji kufanya vizuri kila mechi, makocha wamemaliza kazi yao, jukumu letu wachezaji ni kuhakikisha tunafanikiwa kusaka alama tatu katika kila mchezo ukiwamo dhidi ya Yanga Princess, hautakuwa mchezo rahisi, tutacheza kwa tahadhari kufikia malengo yetu," alisema Violeth.

Kocha Msaidizi wa Yanga Princess, Fred Mbuna, alisema vijana wako salama na wamejiandaa vizuri na mechi hiyo ambayo wataingia 'kikubwa' kuhakikisha wanafuta 'unyonge' mbele ya wapinzani wao.

Mbuna alisema wanaangalia zaidi kusaka matokeo ya leo licha ya Simba Queens kuwa imara katika safu ya ushambuliaji wao wamejipanga vyema kuhakikisha hawaruhusu kufungwa.

"Tunatambua hii ni dabi, ni mchezo mkubwa sana, katika michezo kadhaa tumekuwa hatupati matokeo lakini tumejipanga safari hii tunaenda kufanya kile kilichofanywa na timu ya wanaume," alisema Mbuna.

Bingwa wa ligi hiyo atapata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika Ligi ya Mabingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).




Kocha Msaidizi wa Namungo, Shadrack Nsajingwa (katikati), akiwania mpira dhidi ya nyota wa timu hiyo katika mazoezi ya kujiandaa kuikabili Azam FC kwenye mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA inayotarajiwa kuchezwa Mei 3, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga, Tabora Utd Mei Mosi

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la FA, Yanga watacheza mechi ya hatua ya robo fainali ya michuano hiyo dhidi ya Tabora United ifikapo Mei Mosi kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Taarifa ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), jana limesema mechi tatu za hatua hiyo zitapigwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, CCM Mkwakwani, Tanga na Liti, Singida.

"Mechi ya Yanga dhidi ya Tabora United itachezwa saa 2:30 usiku, ambapo kabla ya hapo zitakuwa zimepigwa mechi mbili, Ihefu ikikwaana na Mashujaa FC, Uwanja wa Liti, Singida, saa 10:00 jioni, kabla ya Coastal Union kuteremka Uwanja wa Mkwakwani, kukipiga dhidi ya Geita Gold, saa 12:15, jioni," taarifa ya TFF ilisema.

Wanafainali wa msimu uliopita, Azam FC wenyewe wanatarajia kushuka dimbani Mei 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex kucheza dhidi ya Namungo FC.

Yanga ilitinga hatua ya robo fainali kwa kuifunga Dodoma Jiji mabao 2-0 wakati Tabora United waliibamiza Singida FG magoli 3-0, Azam yenyewe iliwachapa Mtibwa Sugar mabao 3-0, Ihefu ikawalaza KMC mabao 3-0 na Namungo iliwaondoa Kagera Sugar kwa penalti 5-3.

Mashujaa FC iliendeleza ubabe kwa Simba baada ya kuwaondoa kwa kuwafunga penalti 6-5, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Michezo
Alhamisi Aprili 25, 2024
Nipashe



'Wachezaji walikata tamaa' UKURASA 21



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Maxi Nzengeli, akimtoka nyota wa JKT Tanzania, Matheo Anthony (aliyelala chini), katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam jana. **PICHA: MTANDAO**

# *Yanga yapunguzwa kasi*

**Na Adam Fungamwangwo**

## Mabingwa hao watetezi wanahitaji pointi 14 tu ili kujihakikishia...

VINARA wa Ligi Kuu Bara, Yanga wamepunguzwa kasi katika mbio za kuusaka ubingwa baada ya kulazimishwa suluhu na 'Maafande' wa JKT Tanzania katika mechi kali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo ulioko Mbweni, Dar es Salaam jana.

**Mechi hiyo ilichezwa jana baada ya juzi kushindikana kutokana na sehemu kubwa ya uwanja huo kujaa maji yaliyotokana na mvua zinazoendelea kunyesha Dar es Salaam na Kamisaa wa mchezo, Kamwanga Tambwe, kuuahirisha.**

Matokeo hayo yanaifanya Yanga kupoteza pointi mbili, sasa imefikisha pointi 59, ikiendelea kupepea juu ya msimamo wa ligi huku JKT Tanzania wamepanda nafasi mbili juu, ikitoka nafasi ya 15 na sasa ipo nafasi ya 13 baada ya kufikisha pointi 23.

Mabingwa hao watetezi, Yanga wanahitaji pointi 16 katika mechi zake saba zilizobakia ili kutawazwa mabingwa kwa mara ya tatu, kwa sababu watafikisha pointi 74 ambazo hazitafikiwa na timu yoyote ile.

Azam yenye pointi 54, ikishinda mechi zake sita ikafikisha jumla ya pointi 72, wakati Simba ikishinda mechi zake tisa itafikisha pointi 73.

Hata hivyo, mechi hiyo ilichezwa kwenye uwanja uliojaa matope na kufanya wachezaji kushindwa kuonyesha ufundi, vipaji na ubunifu na badala yake kucheza kwa jinsi unavyoruhusu.

Mara kwa mara wachezaji walishindwa kupiga chenga huku wengine wakianguka wenyewe au kushindwa kukaba kwa urahisi, wakati mwingine kupigwa chenga nyepesi, wakiteleza na kuanguka wenyewe wakati wa kukokota mpira.

Dakika 10 za mwanzo hakuna timu yoyote kufika langoni mwa mwenzake mpaka dakika ya 11, Yanga ilipofanya hivyo kwa shambulizi ambalo lilizaa kona ambayo haikuzaa goli.

Mpira wa kona uliopigwa uliokolewa na mabeki wa JKT Tanzania, lakini ukakwama katika matope mbele ya mshambuliaji, Stephane Aziz Ki, ambaye alipiga shuti kali kwa mguu wa kushoto ukawababatiza tena mabeki, kabla ya kuokoa.

Dakika mbili baadaye, Augustine Okra, alikosa bao, baada ya kichwa alichopiga kuunganisha krosi ya Yao Kouassi kutoka nje kidogo ya lango.

JKT Tanzania ilifika langoni kwa Yanga mara ya kwanza katika dakika ya 15, baada ya George Wawa kuambaa na mpira katika wingi ya kulia, akapiga krosi iliyobabatiza mabeki wa vinara hao wa ligi, nusura mpira ujae wavuni kama si kipa, Djigui Diarra, kuwa makini na kuunyaka mpira huo.

Kuanzia dakika ya 30, JKT Tanzania ilionekana 'kuchangamka' kwa Yanga kufanya mashambulizi kadhaa ambayo yalionekana hatari ingawa hayakuzaa mabao.

Kama wachezaji wa timu hiyo wangekuwa makini wangepata bao dakika ya 34, kupitia kwa Said Ndemla ambaye alikimbia na mpira katika wingi ya kulia na kuingia ndani kidogo kabla ya kuachia shuti kali lililomparaza Diarra, lakini liliambaa pembeni na kutoka nje.

Dakika nne baadaye, maafande hao walifanya shambulio la hatari, ambapo kama si uimara wa beki, Ibrahim Hamad 'Bacca' aliyekuwa akijitosa kuzuia mashuti matatu yaliyokuwa yakipigwa na kumbabua kichwani na mwilini, wangeweza kuandika bao.

Kipindi cha pili Yanga waliingia kwa nguvu kufanya mashambulizi, huku JKT Tanzania nao wakibadilisha mfumo kwa 'kupaki basi'.

Ilikuwa ni dakika ya 57 ambapo Yanga ilikaribia kupata bao kupitia kwa, Maxi Nzengeli, aliyekuwa ndani ya eneo la hatari, akapiga shuti kali lililopanguliwa na kipa, Jacob Suleiman, lakini ulitua mbele ya lango na

INAENDELEA UKURASA 23

# Mo kufanya 'kufuru' usajili mpya 2024/25

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutokuwa na msimu mzuri wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kuwa imeondolewa katika mashindano ya Kombe la FA, Mwekezaji wa Simba, Mohammed Dewji 'Mo' anatajwa ameahidi kukabidhi 'fungu nono' la fedha kwa ajili ya kukamilisha mchakato wa usajili wachezaji wenye ubora watakaoisaidia timu hiyo kufanya vyema kwenye michuano mbalimbali msimu ujao, imefahamika.

Taarifa kutoka ndani ya Simba zinasema Mo ameshaanza kutoa fedha hizo na tayari mchakato wa kuboresha kikosi chao ili kirejeshe heshima na furaha kwa wanachama na mashabiki wake.

Chanzo chetu kimesema kikosi maalum kilichopewa jukumu la usajili na kutafuta wachezaji bora kwa viwango vya juu wameshaanza kazi.

Hata hivyo chanzo hicho kilisema Mo aliwaambia wazi viongozi wa klabu hiyo haridhishwi na viwango vya wachezaji na mwenendo wa timu uliopo kwa sasa, na anataka kuona 'unyonge' huo unamalizika.

"Hivi karibuni Bosi alifanya kikao na viongozi wa Simba lakini pia alikutana na washauri wake ili kujadili mwelekeo wa jinsi ya timu yetu inavyokwenda. Ameona madhaifu na bahati nzuri amezungumza na Benchikha (Abdelhak) na kumweleza anaumizwa na mwenendo wa timu, amewapa watu maalum jukumu la kufanya usajili, kufuatilia wachezaji ambao anahitaji ili kuboresha kikosi," kilisema chanzo chetu.



Kiliongeza mbali na kufanya maboresho, pia wako tayari kuuza wachezaji wao ambao watatakiwa na timu nyingine za ndani na nje ya Tanzania.

"Baadhi ya wachezaji watauzwa na wengine tutaachana nao, hapa mezani tuna ofa Henock Inonga,

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >